




UKURASA 2

## IPP MEDIA ilivyong'ara mchango wa elimu ya afya


Nipashe Spotika

KWA NINI CASEMIRO USAJILI MZURI MANCHESTER UNITED?

CASEMIRO

ISIKUPITE

UKURASA 11

# Nipashe

Jumatatu Agosti 29, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581052

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

## RIPOTI MAALUM

# Raia Ukraine wanavyoishi vijijini Unguja

**WALAZIMIKA** kuzikimbia hoteli, wanakijiji wawapa tabasamu...*Endelea ukurasa wa 4*



Raia wa Ukraine, Vladyslava Yanchenko, akizungumza na mwandishi wa Nipashe (hayuko pichani) katika moja ya migahawa ya kienyeji kijijini Paje, Unguja wiki iliyopita. Kulia ni raia mwenzake wa Ukraine, Viktor Tkachov. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**



UKURASA WA 2

### SHULE YA UHANDISI WA TIBA KUJENGWA CHUONI UDOM

KAMPUNI ya Association of African Economic Development (AFRECO) ya Japan imeonesha nia ya kujenga chuo cha uhandisi wa tiba (School of Medical Engineering) kwa kushirikiana na...

UKURASA WA 3

### KAMPUNI 11 ZA CHINA ZATUA KUONA FURSA ZA UWEKEZAJI

WAWEKEZAJI wakubwa wa kampuni 11 za China wanaoishi Marekani, wamekuja nchini kuangalia fursa za uwekezaji baada ya kuridhishwa na hatua...

UKURASA WA 7

### MAKARANI WAPIGWA MARUFUKU KUREKODI MAHOJIANO SENSA

MKURUGENZI Mkuu wa Ofisi ya Takwimu (NBS) na Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, amesema adhabu anayostahili karani aliyefanya kosa la kupiga picha...

## Bunge laagiza maofisa 30 wa Jeshi Uhamiaji wawajibishwe

UKURASA 3

# Asilimia 86 wafikiwa na makarani sensa

UKURASA 2

MICHEZO RAIS SAMIA AIPONGEZA SIMBA QUEENS UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Kampuni kujenga shule ya uhandisi wa tiba UDOM

**Na Mwandishi Maalum**

KAMPUNI ya Association of African Economic Development (AFRECO) ya Japan imeonesha nia ya kujenga Chuo cha Uhandisi wa Tiba (School of Medical Engineering) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) ili kupunguza tatizo la uhaba wa wataalamu wa tiba na vifaatiba nchini.

Rais wa kampuni hiyo, Tetsuro Yano, alitoa ahadi hiyo juzi alipokutana na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, jijini Tunis, Tunisia ambako anamwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan kwenye Mkutano wa Nane wa Kimataifa wa Wakuu wa Nchi na Serikali unaohusu Maendeleo ya Japan na Afrika (TICAD8).

Yano alisema walipokuja Tanzania, waligundua kuna vifaa vinavyonunuliwa lakini vinashindwa kufanyiwa ukarabati pindi vikipata hitilafu kwa kuwa hakuna wataalamu.

"Kwa kuzingatia hilo, tumeona haja ya kuanzisha chuo cha uhandisi tiba ili tufundishe wataalamu watakaokuwa wakifanya matengenezo ya vifaa badala ya kuagiza mafundi kutoka nje au kuviacha visitumike tena," alisema.

Pia alimweleza Waziri Mkuu kwamba walishapokea maombi kutoka UDOM ya kupatiwa basi la kutoa tiba lenye vifaa mahsusi vya hospitalini (mobile clinic bus) ambalo litakuwa likisaidia kutoa huduma kwenye vijiji vya jirani na chuo hicho.

Mtaalamu kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Sanaa cha Kurashiki cha Japan, Dk. Tomotaka Naramura, alimweleza Waziri Mkuu kwamba wana nia ya kufungua chuo hicho mwaka 2023.

Alisema walikutana na mkuu wa chuo hicho na wakakubaliana kuwa ipo haja ya kuendeleza rasilimali watu kwenye upande wa tiba ili kuwe na wataalamu mahsusi kwa ajili ya vifaa tiba vinavyonunuliwa.

Waziri Mkuu aliwashukuru kwa kuonyesha nia ya kuendeleza sekta ya afya na hasa kwenye eneo la vifaa tiba kwa kuwa linaendana na matarajio ya Rais Samia ya kutaka kuboresha afya za Watanzania kwa kuhimiza ujenzi wa hospitali, vituo vya afya na zahanati.

"Serikali ya Tanzania imeridhishwa na nia ya kampuni yenu ya kuwekeza kwenye uhandisi wa tiba kwani tunawahitaji sana watumishi wa hiyo kada. Hawa watasaidia siyo UDOM peke yake, bali pia Muhimbili, Bugando, KCMC na vituo vingi vya afya ambako serikali imepeleka vifaa tiba," alisema.

Aliwataka waendelee kuwasiliana na Balozi wa Tanzania Japan, Balozi Baraka Luvanda, ili kuhakikisha suala hilo linakamilika.

# Asilimia 86 wafikiwa na makarani sensa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ASILIMIA 86.4 ya Watanzania hadi juzi walikuwa wamehesabiwa katika Sensa ya Watu na Makazi ambayo leo inaingia siku ya saba.

Akizungumza na Nipashe jana, Mratibu wa Sensa Kitaifa kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Seif Kuchengo, alisema pamoja na kwamba leo ni siku ya mwisho, hakuna Mtanzania atakayeachwa bila kuhesabiwa.

"Kilichofanyika kwa sasa kwenye maeneo ambayo makarani wameshakamilisha, tumewapeleka kwenye maeneo ambayo bado ili kuongeza nguvu," alisema.

Mratibu hiyo pia alisema wametoa namba ya simu ili Watanzania ambao hawajafikiwa na makarani wa sensa, wapige simu kutoa taarifa ili wahesabiwe.

"Hata kama siku tulizopanga hizi saba zinaisha kesho (leo), hatutaacha kuhesabu kwa watakaopiga simu kama hawajahesabiwa, lakini tutakapokuwa tunafanya sensa ya majengo pia tukigundua kuna kaya haikuhesabiwa, tutahesabu. Lengo letu ni kila Mtanzania ahesabiwe," alisema.

Kushengo alisema makadirio ya idadi ya watu kwenye sensa ya mwaka huu yaliyotokana na sensa iliyopita, ni kufikia watu milioni 61.3 lakini kuna uwezekano kuongezeka kutokana na sababu mbalimbali na kufikia milioni 64.

Hivi karibuni, mratibu huyo alisema sensa ya majengo itafanyika baada ya siku saba zilizopangwa kwenye sensa ya watu.

"Siku ya nane hadi ya 10 itafanyika sensa ya majengo kwenye majengo yaleyale yanayotumika kuhesabu watu na hatutakuwa na maswali mengi sana, tunahitaji taarifa za majengo tu, basi!" Alisisitiza.

Kwa mujibu wa mratibu huyo, sensa hiyo itafanyika kuanzia Agosti 30 hadi Septemba Mosi mwaka huu ambapo majengo yote nchini yatahesabiwa.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimkabidhi cheti cha shukurani Meneja Uhusiano wa IPP Media, Nancy Mwanyika, baada ya kumaliza mbio fupi na matembezi ya hiari, ikiwa ni sehemu ya Kampeni ya 'Uzazi ni Maisha'. Kampuni ya IPP Media ilikabidhiwa cheti cha ushiriki na kwa mchango wao wa kutoa elimu ya afya kupitia vituo cha ITV, Radio One na East Afrika TV/Radio mwishoni mwa wiki. Katikati ni Mkurugenzi Mkaazi wa AMREF Health Africa, Dk. Florence Temu **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# IPP Media yakabidhiwa cheti mchango elimu afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kupungua na kuepusha vifo vya kinamama na watoto wachanga vitokanavyo na uzazi ni jukumu linalohitaji ushiriki wa kila mtu.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi Uwanja wa Amani mjini hapo, baada ya kumaliza mbio fupi na matembezi ya hiari, ikiwa ni sehemu ya Kampeni ya 'Uzazi ni Maisha' na Kampuni ya IPP Media ilikabidhiwa cheti cha ushiriki, na kwa mchango wao katika kutoa elimu ya afya kupitia vituo cha ITV, Radio One na East Afrika TV/ Radio.

Dk. Mwinyi alisema kuna umuhimu kwa kila mtu mahala alipo, ikiwamo sekta binafsi, mashirika na asasi zisizo za kiserikali kushiriki kikamilifu katika kupunguza na kuepusha vifo vya kinamama na watoto wachanga vitokanavyo na uzazi.

Alisema ili kufikia lengo hilo kuna umuhimu wa kuwaaminisha wajawazito kwamba 'Uzazi ni Uhai' ili waamini kuwa lengo la uzazi ni kuleta maisha mapya duniani na sio kuondoa maisha ya wazazi.

Alisema kuwapo kwa idadi kubwa ya vifo vya kinamama nchini vitokanavyo na uzazi kunachangiwa na changamoto mbalimbali, ikiwamo mifumo ya utoaji huduma za afya, upungufu wa vifaa tiba na dawa, ufinyu wa miundombinu, uchache wa madaktari na wauguzi na suala la mila na utamaduni.

Dk. Mwinyi ambaye aliambatana na mkewe, Mariamu Mwinyi, alitoa takwimu za matukio ya vifo vya wazazi vitokanavyo na uzazi kuwa vimefikia 134 kwa kila wajawazito 100,000 na watoto 37 kwa kila vizazi 1,000.

Alisema hatua ya serikali kujenga hospitali za wilaya pamoja na Hospitali ya Mkoa Mjini Magharibi unalenga kuondoa msongamano wa wananchi wanaofuata huduma katika Hospitali ya Mnazimmoja na Abdalla Mzee mkoani Pemba, ili kupunguza vifo.

Aliwahakikishia wanamichezo walioshiriki mbio na matembezi hayo kuwa serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi kuimarisha mifumo ya utoaji huduma za afya, utoaji wa mafunzo pamoja na kutekeleza mpango uliopo wa kuanzisha Bima ya Afya na kuongeza Bajeti ya Wizara ya Afya.

Dk. Mwinyi alisema amefurahishwa na taarifa kuwa jumla ya vituo 28 vitapata vifaa tiba kati ya 70 vinavyotoa huduma ya mama na mtoto Unguja na Pemba.

"Kwa kutambua juhudi hizo serikali nayo itahakikisha inafanikisha upatikanaji wa vifaa tiba kwa asilimia 60 ya vituo iliobaki," alisema.

Alisema kuwa juhudi za kumarisha huduma za mama na mtoto zinapaswa kwenda sambamba na hatua ya utoaji wa elimu kwa makundi mbalimbali ndani ya jamii.

Alipongeza waandaaji wa kampeni hiyo, AMREF Health Africa, pamoja na wadhamini mbalimbali waliofanikisha shughuli hiyo, ikiwamo Benki ya Taifa ya Biashara (NBC).

Naye Waziri wa Afya, Ahmed Nassor Mazrui, alisema ujio wa kampeni hiyo unathibitisha kwa kiasi gani serikali ilivyojizatiti kushughulikia suala la afya ya mama na mtoto nchini.

Mkurugenzi Mkaazi wa AMREF Health Africa, Dk. Florence Temu, alisema AMREF kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imekuja na kampeni hiyo kwa lengo la kuhamasisha upatikanaji wa vifaa tiba kama nyenzo ya kutatua changamoto za uzazi salama, kuongeza uelewa na hamasa kwa jamii pamoja na ushirikishwaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobaid Sabi, alisema benki hiyo ni muumini mkubwa wa falsafa ya kusaidia jamii, akibainisha kila mwaka hutenga fedha kwa ajili ya kusaidia jamii katika maeneo mbalimbali, ikiwamo afya, elimu, uwezeshaji na mengineyo.

Kampeni ya 'Uzazi ni Maisha' iliyobeba ujumbe wa changia vifaa tiba kwa uzazi salama iliwashirikisha wanamichezo na vikundi mbalimbali vya mazoezi Zanzibar, ilianzia Maisara na kumalizikia Uwanja wa Amani.

# Kampuni 11 za China zatua kuona uwekezaji

**Na Romana Mallya**

WAWEKEZAJI wakubwa wa kampuni 11 za China wanaoishi Marekani, wamekuja nchini kuangalia fursa za uwekezaji baada ya kuridhishwa na hatua zilizochukuliwa na serikali.

Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda kwa upande wake amewahakikishia wawekezaji hao kuwa Tanzania ina amani, utulivu na viongozi wake wana utayari wa kuhakikisha uwekezaji unafanyika.

Alisema kutokana na utayari huo kuna chombo kinachosimamia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kuhakikisha hakuna urasimu watakaoupata.

Akifungua mkutano uliowakutanisha wawekezaji hao, TIC, Chama cha Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima Tanzania (TCCIA), serikali na wadau wengine, mwishoni mwa wiki, alisema wageni hao wamekuja nchini kuangalia fursa za kuwekeza na tayari wameonyesha nia hiyo.

"Kuwapo kwa fursa ni jambo moja, yapo mambo ya msingi kwa mwekezaji anapotaka kuja kuwekeza katika nchi yoyote, kwanza ni amani ya taifa husika. Kwa Tanzania tunamshukuru Mungu kwamba jitihada kubwa zimefanyika na nchi ina utulivu na amani mpaka sasa.

"Pili, kunahitajika utayari kutoka kwa viongozi ambao ndiyo wanaoongoza Taifa, tulichofanya ni kuwahakikishia kuwa, Tanzania hilo sio jambo la kwamba linajadiliwa, lipo kwa viongozi waliotangulia hata walioko sasa chini ya Rais Samia Suluhu Hassan," alisema.

Aliwaeleza kuwa maelezo na msisitizo mkubwa wa viongozi upo kuhakikisha uwekezaji ni jambo linalotakiwa kupewa msukumo mkubwa.

Pinda alisema Tanzania kuna TIC ambayo imeondoa urasimu kwa wawekezaji na kuna maeneo mengi ya kuwekeza kama kwenye utalii, kilimo, ujenzi, mawasiliano, viwanda vya usindikaji wa mazao mbalimbali.

Aliwashukuru kwa kuichagua Tanzania kama sehemu muhimu ya kuwekeza na kwamba milango iko wazi muda wote.

"Tanzania tuna maeneo mengi ya uwekezaji na Rais Samia Suluhu Hassan aliamua kuandaa filamu maalum ya The Royal Tour ambayo ndani yake inaonyesha maeneo mbalimbali ya vivutio tulivyonavyo. Baada ya filamu hii tumeshuhudia watalii wakija nchini," alisema. Kaimu Mkurugenzi Mtendaji TIC, John Mnali, alisema wamekutana na kundi la wafanyabiashara hao ambao wanatafuta fursa za uwekezaji Tanzania.

"Kupitia mazungumzo ambayo tumeanza kufanya wameonyesha nia ya kuwekeza katika sekta ya utalii kwa kujenga hoteli za kitalii zenye hadhi ya nyota tano, kujenga kumbi kubwa za mikutano ambazo zitakutanisha watu hasa ile mikutano ya kimataifa, wameonyesha nia ya kuwekeza katika utengenezaji wa dawa za binadamu, kilimo na wapo wanaotaka kuwekeza kwenye filamu wapo wataalamu wamekuja kutoka Hollywood ambao wapo kwenye huu msafara," alisema. Mnali alisema jukumu la TIC ni kukaa nao na kuwasaidia pale watakapofikia hatua ya kuhitaji vibali na leseni mbalimbali.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wa China nchini Tanzania, Jinfeng Zhu, aliwaeleza wafanyabiashara hao kuwa Rais Samia amewaalika wawekezaji duniani kuja Tanzania kuwekeza katika sekta tofauti.

Pia aliwaeleza kuwa Tanzania ina fursa nyingi za kuwekeza na serikali imefanya maboresho makubwa kwenye mazingira ya kufanya biashara na kuwataka wachangamkie hilo kwani ardhi ya nchi ni kubwa.

Aliwataka wafanyabiashara wa Tanzania wanaoagiza bidhaa nchini kwao kwa ajili ya usalama wa mizigo yao wapitie kwenye chama hicho ili wasidhurumiwe.

# Bunge laagiza maofisa 30 wa Uhamiaji wawajibishwe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeagiza maofisa 30 kati ya 41 wa Jeshi la Uhamiaji waliobainika kusababisha hasara ya Sh. bilioni 2.5 kutokana na upotevu wa stika za visa, wachukuliwe hatua na fedha hizo zirejeshwe.

Vilevile, kamati hiyo imeagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) afanye ukaguzi maalum wa mfumo wa visa (e-visa) unaotumika sasa, ili kubaini dosari zilizokuwapo kwenye mfumo wa awali kama zimedhibitiwa na hakuna upotevu mwingine wa fedha.

Makamu Mwenyekiti wa PAC, Japhet Hasunga, alibainisha hayo jana alipozungumza na Nipashe jijini hapo kuhusu maagizo yaliyotolewa na kamati hiyo baada ya kuhoji fungu la Uhamiaji mwishoni mwa wiki kutokana na hoja za ukaguzi zilizotolewa na CAG.

Alisema ukaguzi maalum wa CAG ulibaini kulikuwa na stika za visa feki ambazo walikuwa wamezitoa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) na mfumo wao waliokuwa wanautumia wa visa ukawa hauonani na mfumo wa usalama wa ndege.

"Hali hiyo ilisababisha watu 33,558 wakawa wamepata visa lakini fedha zao zilikuwa hazionekani kwenye mtandao na taarifa zao zikawa zimefutika,

"Yaani hazikuonyesha kama zimeingia kwenye mfuko wa serikali, uchunguzi ulibaini watu 41 wamehusika na kusababisha hasara ya Sh. bilioni 2.5.

"Yalitolewa maagizo kwamba wale watu waliohusika na upotevu wa hizo stika na kufanya mfumo uwe mbovu wachukuliwe hatua na ripoti ya ukaguzi maalum ilibainisha maofisa 41 wa Uhamiaji, kati yao waliochukuliwa hatua na kushtakiwa ni 11 tu," alisema.

Hasunga ambaye kitaalamu ni mhasibu mwenye hadhi ya CPA, alisema kamati imeagiza Ofisa Masuuli achukue hatua za kisheria na kinidhamu kuhusu watumishi hao wote waliobainika kwenye ukaguzi huo. "Warudishe hizo fedha kwa sababu hata wengine wote wapo kazini, wamehamishwa. Kwa hiyo, warudishe fedha hizo zote," kiongozi huyo wa kamati alibainisha maagizo yao.

Hasunga pia alisema kamati imeagiza kufanyike marekebisho ya hesabu zao ambazo zimeonekana zina makosa ili kuonyesha sura halisi ya hesabu, akisisitiza kuwa wanatakiwa kuwasilisha majibu kwa kamati leo kabla ya saa 10 jioni.

"Wahakikishe wanajibu hoja zote za ukaguzi zilizobainishwa kwenye ripoti na zifungwe ndani ya mwaka huu wa fedha, hizo hoja zilikuwa wanaonekana wanafanya ununuzi bila kuzingatia taratibu, wamenunua viwanja, miradi mingine imechukua muda mrefu, maagizo ya Bunge hayajatekelezwa ipasavyo, viwanja ambavyo havina hati vishughulikiwe, majibu yatolewe na hoja zifungwe kwa mujibu wa taratibu,"alifafanua.

Kamati hiyo inafanyia kazi ripoti ya ukaguzi wa CAG kwa mwaka wa fedha 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12, mwaka huu pamoja na ufuatiliaji wa mapendekezo ya nyuma ya Bunge na CAG.



## VIKTOR & VLADYSLAVA

# Watalii Ukraine waliohamia kijijini Unguja

## ■Wapasujudu kwa kila hali, mmoja awa mpangaji kijijini Paje, mama na mtoto wajenga Kizimkazi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UNAPOYATAJA maeneo ya Kizimkazi ambako ni umbali wa Km 56, hali kadhalika Paje Km 48.7 kutoka mjini Unguja, kwa sifa zote ni kijijini na wakazi wake ni waswahili hasa wa Zanzibar, maisha yao yakiwa ni ukulima wa gharama za chini.

Kuna nyumba nyingi zilizoezekwa kwa makuti, pia kujengewa uzio wa makuti unaozuia vumbi la upepo mkali kutoka pwani.

Lakini kwa ambaye hajafika maeneo hayo tangu mwanzoni mwa mwaka huu, mara moja anaweza akapigwa na butwaa kukuta kwamba sehemu ya wenyeji wake hao waswahili wa Unguja, ina jamii ya raia wa kigeni, wenyeji wakiwaita kwa jina la 'wazungu', nao wamejichanganya huko na ni wanakijiji rasmi wa Kizimkazi na Paje, wakiishi maisha kama ya wenyeji wao kwa sifa zote na wamehusudu hasa mfumo huo.

Hao ni wenyeji raia wa Ukraine walioyapenda makazi na wakakarimiwa na sasa nao ni wana Unguja.

Viktor Tkachov (45), mhandisi wa umeme ambaye tatizo la vita nyumbani kwao lilimkuta akiwa katika shughuli za utalii Unguja, anaiambia Nipashe kwamba sababu yake ya kuwa Unguja ni shida, lakini ghafla imegeuka kuwa mapenzi makubwa, hata moyo wake unasita kuondoka.

Vivyo ilivyo kwa dada yake, Vladyslava Yanchenko (23), ambaye yuko kijijini Kizimkazi na mama yake, anasimulia sura hiyo ya upekee wa Wazanzibar unaogusa hisia zote za udugu, sasa anafungua milango kwamba iwapo akitokea mwenye utayari, basi yuko tayari kuunda familia naye hapo hapo Unguja.



Raia wa Ukraine, Vladyslava Yanchenko, akizungumza na mwandishi wa Nipashe (hayuko pichani) katika moja ya migahawa ya kienyeji kijijini Paje, Unguja wiki iliyopita. Kulia ni raia mwenzake wa Ukraine, Viktor Tkachov. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

Ziara hiyo maalum ya Nipashe vijijini huko siku chache zilizopita, iliwashuhudia namna wageni wenyeji hao wakijichanganya huku na kule, si tu kwamba wanaishia katika mazungumzo, bali wamezama katika milo na ukanda mpana wa utamaduni wa makazi hayo mapya ya Unguja.

Kila mahali Nipashe ilikotembelea, iliwakuta wakiwa katika harakati kubwa za kuvunja kikwazo cha lugha, kila mmoja akipigana kujua Kiswahili na mizizi yake.

"Wanakajiji hawajui Kiingereza, hivyo ninajifunza Kiswahili ili niwasiliane nao vizuri na nimeanza kujua baadhi ya maneno polepole," anasema Viktor, mwanakijiji mpya wa Paje.

Vikirejewa vita kati ya Russia na Ukraine mnamo Februari 24, mwaka huu vilipoanza, wawili hao tayari walikuwa na siku chache Unguja kwa ziara ya kitalii, wakiwa ni miongoni mwa watalii 1,200 kutoka Ukraine.

Mkurugenzi wa Uratibu Shughuli za Utalii kutoka Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Omar Suleiman Mohammed, anasema kundi lingine walitawanyika kwingineko, isipokuwa Viktor, Vladyslava na wenzao 10 walibaki nchini.

Hata hivyo, katika kundi hilo, wako sita waliokuwa wamekwama kulipia gharama za usafiri, walisaidiwa na Serikali ya Zanzibar kuelekea walikonuia.

Wakabakia 12 walioonekana kuwa wapenzi kindakindaki wa visiwani, hawakutaka kuondoka na katika hatua ya kwanza Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi alielekeza wapewe viza za bure na kuzitaka hoteli ziwapungie makali ya gharama.

Kadri muda ulivyosonga, makali ya gharama na mazoea yao uswahilini, yakaanza kuleta historia ya mmoja baada ya mwingine kuanza kuwa mpangaji au mkazi wa uswahilini, kuchanganyika na wenyeji na kuishi maisha ya wasifu wa mitaani Unguja.

Katika hilo Viktor anaeleza: "Vita vimesababisha tushindwe kurejea nyumbani. Kwa sasa tunaishi na wanakijiji kwa sababu hatuna fedha ya kujikimu kama watalii wa kuishi hotelini."

Kauli yake inaendana na pale Nipashe inapomshuhudia akiwa kwa mamalishe wa kijijini Paje, akipata mlo wa asubuhi, chapati na supu, akichanganyika na wanakijiji.

Mwenzake, Vladyslava, anakwenda mbali zaidi katika uhusiano wake na wenyeji wa Unguja kwani hata mapema kabla ya vita, anaiambia Nipashe alishanunua ardhi kwa ajili ya uwekezaji.

Hapo ndipo pameshuhudiwa nyumba ndogo aliyoamua kuijenga ili kujisitiri yeye na mama yake mzazi.

"Mimi ninaishi katika nyumba yangu Kizimkazi lakini haina mazingira mazuri. Nilitarajia nijenge nyumba kwa ajili ya kuwekeza lakini nimeshindwa, biashara zangu zimevurugika na sina fedha ya kuziendeleza," Vladyslava anabainisha madhara ya vita.

Makazi hayo kwa ujumla yana sifa zote za mtu anayejikimu kuondoka na adha ya kukosa makazi, ikiwa ni nyumba ambayo haijasakafiwa, haijanakishiwa ukutani na maboresho mengine yanayotarajiwa kwenye nyumba bora.

Hassan Ali, mkazi wa Kijiji cha Kizimkazi, anamtaja Vladyslava kwa sifa za mtu anayependa kujichanganya na wanakijiji, mcheshi, mpole na asiye na majivuno na anapenda kujifunza Kiswahili.

### HISTORIA YAO

Vladyslava anasema alifika kitalii Zanzibar kwa mara ya kwanza mwaka 2020, ndipo alipovutiwa na uwekezaji. Hata hivyo, anasita kutaja taaluma yake na anaeleza amezaliwa miaka 23 iliyopita.

Anasema amevutiwa na maisha ya Zanzibar kutokana na ukarimu wa watu wake na anapata ushirikiano mkubwa kutoka kwa majirani na wanakijiji.

"Zanzibar ni paradise (peponi) na inaweza kuwa kivutio cha watalii wengi lakini inahitaji teknolojia ya kisasa. Watalii wana fedha nyingi ambazo wanaweza kuleta Zanzibar," anasema.

Kaka yake, Viktor, ni mhandisi wa umeme aliyezaliwa katika Mji wa Odessa na kukulia Mji Mkuu wa Ukraine, Kiev, anajivunia kuishi kijijini Paje Mkoa wa Kusini Unguja, akitamba sasa ana maisha ya kawaida sawa na Mzanzibar mwenye kipato cha chini.

"Gharama ya chakula cha asubuhi haizidi Sh. 3,000. Leo nimekula chapati mbili na supu ya ng'ombe... maisha yanaendelea," anasema.

Hata hivyo, Viktor anasema hana shughuli inayomwingizia kipato kwa sasa, hivyo anaendelea kutumia fedha yake ya akiba ambayo inakaribia kuisha.

Anaishukuru serikali kwa kuwapa hifadhi na kuwasaidia kupata viza ya kuendelea kuishi visiwani humo bila gharama.

### KUTOKA SMZ

Mkurugenzi wa Uratibu Shughuli za Utalii kutoka Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Omar Suleiman Mohammed, anafafanua kuwa raia wa Ukraine 1,200 walikuwa Zanzibar kwa shughuli za utalii wakati vita vinatokea nchini kwao.

Anasema wakati vita vinaendelea, wengi wao waliondoka na kuelekea mataifa mbalimbali ya Ulaya kwa gharama zao, sita walisaidiwa usafiri na serikali na 12 wamebaki Zanzibar.

"Kati ya 12, wapo waliokodi nyumba na wengine wamepewa hifadhi na serikali inawasaidia gharama za viza ili kuendelea kubaki nchini," anasema.

Ofisa Uhusiano kutoka Jeshi la Uhamiaji Zanzibar, Sharif Bakar, anasema wanashirikiana na Kamisheni ya Utalii Zanzibar inayowapatia taarifa za watalii wa Ukraine waliopo nchini.

Anasema wameendelea kuwapa viza bila gharama na hakuna aliyekataliwa na wapo waliongezwa muda wa viza zao kuishi nchini.

Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa (UN) vita vya Urusi na Ukraine vilivyoanza Februari mwaka huu, vimesababisha zaidi ya raia milioni 6.7 wa Ukraine kukimbia nchi hiyo.

Vita hivyo pia vimesababisha mzozo wa kiuchumi katika nchi nyingi duniani kutokana na kupanda gharama za mafuta na bidhaa za chakula kutokana na chi hizo mbili kuwa wazalishaji wakuu wa bidhaa hizo.

Zanzibar pia imeathiriwa na vita hivyo hasa katika sekta ya utalii ambapo watalii kutoka Ukraine walikuwa wakiingia kwa wingi visiwani hapo.

Mnamo Februari 24 mwaka huu, Russia iliivamia Ukraine kijeshi ikiwa ni matokeo ya msuguano mkali kati ya nchi hizo ulioanza mwaka 2014.

UN imeshaweka wazi kuwa vita hivyo vimesababisha kuwapo idadi kubwa zaidi ya wakimbizi (milioni 6.7) duniani tangu Vita vya Pili vya Dunia, kiwango hicho kikiwa ni sawa theluthi moja ya wakazi wote wa Ukraine.

TANGAZO

## INVITATION TO TENDER FOR PROVISION OF A WAREHOUSE FACILITY - REF. NO. WHFR/1-22/08

**Introduction**

**MIC Tanzania Public Limited Company associated with its commercial brand Tigo is an innovative telecommunication company in the country, distinguished asa fully-fledged digital lifestyle brand. With over 10 million registered subscribers, MIC Tanzania Public Limited Company directly and indirectly engages with over 300,000 Tanzanians including an extended network of customer service representatives, mobile money merchants, sales agents and business partners.**

### Invitation to apply for MIC Tanzania Public Limited Company Retail Business Partnership

MIC Tanzania PLC invites reputable limited companies or individuals in Tanzania to bid for provision of a warehouse facility for lease. The Warehouse will be used for keeping telecom equipment, spare parts, marketing promotional/merchandise materials, documents, furniture, ICT and office equipment.

### General Criteria

i). **Size:** 2,500 to 3,000 square meters.
ii). **Preferred Locations:** Mikocheni area, Mwenge area, Ubungo, Mabibo, Kurasini, Chang'ombe, Keko, along Nyerere Road between the junction of Nyerere/Kawawa Road (VETA) and JNIA terminal
iii). **Access to the facility:** Easily accessible (especially with big trucks).
iv). **Outdoor Space:** Enough space that allows long vehicles to turn easily.
v). **Flooding:** Must be in area that cannot be flooded.
vi). **Minimum roof height:** 18 meter high.
vii). **General building condition:** internal and external must be in a very good condition.
viii). **Power connectivity:** Must be connected to grid power (Tanesco), a standby generator will be an added advantage.
ix). **Water:** Must have running water.
x). **Availability:** The warehouse must be available from 1st January 2023

### Other terms and conditions

i). Evaluation of applicants will be conducted as per MIC Tanzania PLC pre-set selection criteria.
ii). Selection criteria will be as per MIC Tanzania PLC set criteria.
iii). Only selected applicants will be contacted, and no reasons shall be provided to unsuccessful applicants.

### How to apply

i). Submit your proposal showing how the proposed warehouse meets the criteria above along with copies of proof of ownership and photos of the facility
(internal and external surroundings).

| **Tender Address:** | Tenderer shall submit signed proposal electronically by e-mail to **joshua.nyagol@tigo.co.tz** |
|---|---|

**Submission:** Deadline for submission is 05:00pm East African Time on 05$^{th}$ September , 2022.
No tender fee will be charged

217016902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Maandalizi Simba Queens CAF sasa yaanzie ilipoishia CECAFA

**KWA** mara ya kwanza katika historia ya nchi hii, timu ya Wanawake ya Klabu ya Simba, Simba Queens, imekuwa ya kwanza kutoka Tanzania kufuzu kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa ngazi ya klabu itakayofanyika Oktoba mwaka huu nchini Morocco. Simba Queens imekata tiketi hiyo baada ya kuibuka mabingwa wa michuano ya kuwania kushiriki fainali hizo za Afrika kwa Wanawake kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), iliyomalizika Jumamosi iliyopita hapa nchini.

Kwa mantiki hiyo, Simba Queens sasa itakuwa timu pekee itakayouwakilisha Ukanda wa CECAFA kwenye michuano hiyo ya Afrika ambayo itafanyika nchini Morocco Oktoba mwaka huu ikishirikisha jumla ya timu nane.

Timu sita kati hizo nane, zinapatikana kutoka kanda tofauti za Afrika ambapo kwa CECAFA rasmi sasa ni Simba Queens, Ukanda wa COSAFA ni Green Buffaloes ya Zambia, Ukanda wa UNAF ni Wadi Degla ya Misri, wakati Ukanda wa WAFU A ni Determine Girls ya Liberia. Bado kanda mbili hazijapata wawakilishi rasmi, ambazo ni Ukanda wa WAFU B ambapo bingwa atapatikana Septemba 2, nchini Ivory Coast huku Ukanda wa UNIFFAC bingwa akitarajiwa kupatikana Septemba 4, mwaka huu nchini Cameroon.

Ikumbukwe pia kuna timu nyingine mbili zilizoingia moja kwa moja ili kufanya idadi kuwa nane, ambazo ni bingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake nchini Morocco, AS FAR Rabat, iliyoingia kama timu mwenyeji pamoja na Mamelod Sundown ya Afrika Kusini, ambayo ni washindi wa pili wa COSAFA walioingia kama bingwa mtetezi.

Kwa orodha hiyo tu ya awali kabla ya kupatikana timu mbili shiriki katika fainali hizo za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Upande wa Wanawake, inaonyesha si michuano rahisi hata kidogo na yanahitajika maandalizi makubwa kwa wawakilishi wa Tanzania, Simba Queens. Hata hivyo, kwa ubora ulionyeshwa na Simba Queens kwenye kinyang'anyiro cha upande wa CECAFA kuwania kufuzu fainali hizo, tunaamini kama maandalizi yataanzia hapo ilipoishia na kufanikiwa kutwaa ubingwa huo, haitatuangusha katika michuano ya CAF. Matarajio hayo makubwa kwetu yanatokana hasa na ubora ulioonyeshwa na wachezaji wa Simba Queens kwa kushinda mechi zote tano kuanzia hatua ya makundi hadi fainali ilipotwaa ubingwa huo wa CECAFA Jumamosi iliyopita.

Lakini si hilo tu, bali pia kama timu ilionyesha ubora zaidi kuanzia safu ya ulinzi hadi ya ushambuliaji, kwani iliruhusu bao moja tu huku ikifunga jumla la mabao 18, hivyo Simba Queens si ya kubeza hata kidogo, ingawa inatakiwa pia itambue sasa inakwenda kukutana na mabingwa kutoka kila kanda.


Kutokana na hilo, ndilo linalotufanya kuwakumbusha kuanzia wachezaji, benchi la ufundi la timu hiyo pamoja na uongozi mzima wa klabu ya Simba, kuhakikisha yanafanyika maandalizi makubwa zaidi kuelekea michuano hiyo kwani tunachotaka kukishuhudia nchini Morocco ni kuona timu hiyo ikifika fainali na kutwaa taji hilo.

Tunaamini hilo linawezekana kama kila mmoja katika timu hiyo atabeba majukumu yake ipasavyo kuanzia nje ya uwanja na ndani ya uwanja husuan kuitafutia mechi nyingi na kubwa zaidi za kirafiki ili kuwaweka wachezaji fiti kuelekea fainali hizo.

Ni wazi michuano ya CECAFA iliyomalizika, imeonyesha ni wapi ambapo panavuja kuelekea fainali hizo za Afrika, hivyo katika kipindi hiki cha mwezi mmoja wa ushee, tunaamini benchi la ufundi linaweza kutafuta suluhisho kwa kuangalia namna ya kupaziba ili kukiimarisha kikosi chao.

Lengo letu ni kuona Simba Queens inatangaza vema soka letu kupitia michuano hiyo mikubwa zaidi barani Afrika kwa ngazi ya klabu kwa upande wa wanawake, lakini ni wakati wa wachezaji kila mmoja kwa wakati wake kujituma na kutozembea mazoezini, kwani kupitia fainali hizo za CAF, ni sehemu sahihi kwao kujitangaza na kupata klabu kubwa nje na ndani ya Afrika kwa maslahi yao binafsi na taifa pia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba Queens iwe chachu ya kipaumbele soka la wanawake

Na Adam Fungamwango

**HAIKUWA** ajabu kubwa sana kwa Simba Queens kutwaa ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) kwa Wanawake, mwaka huu kwa jinsi ambavyo walijipanga na kuwekeza.

Baada ya mwaka jana kuishia hatua ya nusu fainali nchini Kenya, viongozi wa Simba walisema walijifunza kutokana na makosa, na kujua tatizo liko wapi.

Walisema walihitaji kuwekeza hasa kwa kusajili wachezaji wengine wenye uwezo na wazoefu wa michuano mikubwa ya kimataifa.

Hayakuwa maneno matupu, walifanya usajili mkubwa kwa kushusha vifaa kama Vivian Corazone ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Kenya, anayechezea pia Timu ya Taifa, Kenya Starlets.

Wengine ni Filomena Abakar kutoka nchini Ghana, Olaiya Barakat kutoka Nigeria, Daniel Ngoi Mkongomani aliyekuwa akiichezea Yanga Princess msimu uliopita na wengineo wengi.

Kikubwa ni kwamba benchi la ufundi liliwaambia viongozi kuwa linahitaji baadhi ya wachezaji wenye maumbile makubwa na nguvu kwenye baadhi ya nafasi ili kuendana na soka la nchi kama Kenya na Uganda.

Timu za Kenya na Uganda ndizo zilionekana kuwa tishio kwa Simba Queens msimu uliopita kutokana na wachezaji wake wengi kuwa na miili mikubwa na nguvu.

Na kweli Vihiga Queens ya Uganda ndiyo iliyotwaa ubingwa na kwenda kuuwakilisha Ukanda wa CECAFA kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita. Hata msimu huu, timu iliyotinga fainali ni She Corporate pia ya Uganda ambayo ilitoa upinzani mkali kwenye mechi ya fainali juzi kutokana na aina yake ya mpira kiasi cha bingwa kushinda bao 1-0 la mkwaju wa penalti.

Ni kwa sababu tu msimu huu Simba Queens nayo ilikuwa imejipanga kisawasawa kwa kukusanya wachezaji kutoka pande mbalimbali za Afrika na kulifanyia kazi suala ya kuwa na baadhi ya wachezaji wenye miili mikubwa na nguvu.

Nasema haikuwa ajabu sana kwa sababu hata msimu uliopita Simba Queens nchini Kenya ilikuwa timu tishio, tatizo lilikuwa ni hilo tu, na likafanyiwa kazi, hivyo haikuwa na sababu kuwa iukose ubingwa msimu huu kwa sababu nyingi tu.

Kwanza bado ina wachezaji wengi waliokuwapo msimu uliopita, hivyo wamezoeana, pia inacheza nyumbani huku safari hii ikiwa ina 'mkwanja' mkubwa uliotolewa na Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan ambaye tangu msimu uliopita aliahidi kuwa atadhamini michuano hiyo ambayo kwa sasa kwa heshima yake inaitwa 'Samia Cup.'

Kiasi cha Dola 60,000 za Kimarekani zilikuwa zinashindaniwa, bingwa akitoka na Dola 30,000, hivyo timu ya Tanzania haikutaka kumwangusha Rais Samia kwani zaidi ya nusu ya pesa hizo zilienda kwenye klabu za nje ya nchi msimu uliopita.

Niwapongeze Simba Queens kwa sababu hawakumwangusha Rais Samia kwani kiasi cha pesa alichotoa hakikwenda bure, faida yake pamoja na kwamba nusu imebaki Tanzania, lakini nchi yake ndiyo itawakilisha ukanda wote wa CECAFA kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Ushindi wa Simba Queens sasa uwe chachu kwa timu zote kuwekeza kwenye soka la wanawake. Imeonyesha kwamba mpira siyo siasa na kuhusiana kwa vitu visivyo na tija, bali yeyote atakayewekeza fedha kwenye maeneo sahihi atapata ushindi na faida zingine.

Kwa bahati mbaya sana wakati michuano hiyo inachezwa, kwenye jezi ya wachezaji wa Simba Queens hakuonekana mdhamini yoyote kifuani. Inadaiwa kuwa udhamini wa timu ya wanaume hauingiliani na ule ya wanawake. Wanawake nao walitakiwa wawe na mdhamini wao.

Kampuni nyingi zimeonekana bado kusita kudhamini soka la wanawake, lakini kwa hili watajiona kuwa walikosea. Ilikuwa ni njia yao ya kujitangaza vema wao na biashara zao.

Michuano hii iliangaliwa na watu wengi sana siyo nchini Tanzania tu, bali hata nje ya nchi ambako wachezaji wa timu hizo wametokea kwa sababu ilikuwa inaonyeshwa laivu. Nadhani sasa kampuni zitakuwa zimeamka na kuamini kuwa soka la wanawake nalo nchini linakua.

Rais Samia tayari ameanza kwa kudhamini, tunataraji kuona kampuni nyingine zikijitosa kusapoti kwa kuwadhamini wawakilishi wa Tanzania na CECAFA, Simba Queens, pamoja na Ligi Kuu ya Wanawake kwa jumla.

Kwa jinsi umati ulivyokuwa umejitokeza kwenye mechi ambazo Simba Queens inacheza, inaonyesha kuwa soka la wanawake limeanza kuwa na mvuto kwa mashabiki wengi. Kwa maana hiyo klabu zingine zinatakiwa kuwekeza sasa kama timu za wanaume, na kuacha kutaka kupitia njia za mkato.

**HABARI KITAIFA**

# DCI achukizwa ongezeko la ukatili dhidi ya watoto

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MKURUGENZI wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Ramadhani Kingai, ameeleza kuchukizwa na matukio ya ukatili dhidi ya watoto wadogo yanayoendelea kuripotiwa nchini.

Alibainisha hayo mwishoni mwa wiki kwenye hafla ya Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Shinyanga ya kutunuku vyeti vya pongezi kwa kikosi kazi cha mahakimu sita ambao wamejitolea kufanya kazi ya kushughulikia mrundikano wa mashauri mahakamani.

Alisema baadhi ya wazazi wanasahau malezi ya watoto wao na wengine kuwatelekeza na kusababisha kuingia kwenye mikono ya watu waovu na kisha kuwanajisi na wengine kulawitiwa.

"Kuna tukio moja la mtoto wa miaka 15 limetokea huko Mtwara, yeye alitelekezwa na wazazi wake, akaachiwa wadogo zake, ndiye akawa mlezi wao, mbinu aliyotumia ni kutafuta wanaume ili wampatie pesa, wanaume wengine akawa anawatimizia mahitaji yao na wengine kutowatimizia, ndipo siku moja akalawitiwa na kuuawa," alisema Kingai.

Alitumia fursa hiyo kuwataka viongozi wa dini kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wawe na hofu ya Mungu na kuacha vitendo vya ukatili na uhalifu ili nchi ibaki kuwa salama.

Alisema kwa sasa nchini matukio makubwa ya uhalifu ya kusisimua yamepungua na kubaki ya mauaji ya wivu wa kimapenzi, ulevi, ushirikina na kujichukulia sheria mkononi.

Katika hatua nyingine Kingai, aliwataka mahakimu katika utekelezaji wa majukumu yao, watangulize uzalendo na uadilifu ili haki itendeke kwa wananchi wote na kupunguza vitendo hivyo vya ukatili na uhalifu.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Shinyanga, Athumani Matuma, alitaja vikwazo vinavyowakabili mahakimu kwenye kutekeleza majukumu yao ni mashahidi kutofika mahakamani na wengine kuogopa kutoa ushahidi na uhaba wa waendesha mashtaka.

Alisema baadhi ya kesi zimekuwa zikifutwa kutokana na kukosa ushahidi, hasa za matukio ya ukatili dhidi ya watoto na kubainisha kuwa kesi hizo zinapofutwa, watu wemekuwa wakilalamika na kueleza kuwa wao hawafanyii kazi hisia za watu, bali ni ushahidi.

Alitoa wito kwa wananchi wa mkoani humo kutumia mahakama kutafuta haki zao na kuacha kujichukulia sheria mkononi, ambapo kwa sasa wameboresha huduma kwa kushughulikia mashauri haraka na hakuna tena kuchukua muda mrefu kama zamani.

# Serikali ya Japan yaahidi kutoa mabilioni Afrika

**Na Mwandishi Maalum**

SERIKALI ya Japan imeahidi kutoa dola za Marekani bilioni 30 ili kuziwezesha nchi za Afrika kutekeleza miradi ya maendeleo na kutunza mazingira.

Ahadi hiyo ilitolewa juzi na Waziri Mkuu wa Japan, Fumio Kishida, alipowasilisha hotuba yake kwenye Mkutano wa Nane wa Kimataifa wa Wakuu wa Nchi na Serikali unaohusu Maendeleo ya Japan na Afrika (TICAD8) unaofanyika jijini Tunis, Tunisia.

Akizungumza kwa njia ya mitandao, Kishida alisema kiasi hicho cha fedha kitatolewa kwa kipindi cha miaka mitatu ili kutunza mazingira, uwekezaji hasa kwa vijana, sekta za afya, viwanda na elimu. "Kwa kuanzia, Japan itaanzisha 'Japan's Green Growth Initiative with Africa' ambapo itatoa dola za Marekani bilioni nne kwa taasisi za umma na za binafsi barani Afrika ili kuziwezesha kutekeleza mpango huo," alisema.

Kuhusu kuboresha maisha ya Waafrika, Kishida alisema kupitia Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) watatoa dola za Marekani bilioni tano ambazo zinajumuisha mkopo mpya wa dola za Marekani bilioni moja zinazolenga kuzisaidia nchi hizo kumudu madeni.

Alisema janga la corona limetoa funzo kuwa kuna haja ya kujiandaa kukabiliana na magonjwa ya mlipuko, hivyo serikali yake itachangia dola za Marekani bilioni 1.08 ili kuiwezesha Afrika kukabiliana na UKIMWI, kifua kikuu, malaria na kuimarisha mifumo ya afya.


**KUPOTEA KWA CHETI**



**ANNA MWAIPOPO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0222/0013** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ZANAKI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2007 . kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/CHU/RB/339723/2022**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KAGERA LILILOPO BUKOBA**

**MAOMBI NA: 34/2022**

**JULIAN JOHN ICHULIKA ......................................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**1. RICHARD MUCHUNGUZI**
**2. ERICK APPOLINARY**
**3. VICTOR GERVASE..........................................MJIBU MAOMBI**

**KWA: RICHARD MUCHUNGUZI**
**ERICK APPOLINARY**
**VICTOR GERVASE (POPOTE MLIPO)**

Mnaarifiwa /unaarifiwa kuwa maombi Na. 34/2022 yamepangwa kutajwa tarehe 13/10/2022 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza P.J. Makwandi saa 2:00 asubuhi. Hivyo, mnaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yenu na hukumu kutolewa.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Baraza hili leo terehe 17/08/2022

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

117016302


# Makarani wa sensa wapigwa marufuku kurekodi mahojiano

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

MKURUGENZI Mkuu wa Ofisi ya Takwimu (NBS) na Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, amesema adhabu anayostahili karani aliyefanya kosa la kupiga picha na kurekodi video wakati Sensa ya Watu na Makazi ni faini ya Sh. milioni mbili, kifungo cha miezi sita au vyote kwa pamoja.

Alibainisha hayo jana akiwa katika ukaguzi wa utekelezaji wa kazi hiyo kijijini Tosamaganga, Kitongoji cha Ipamba, Kata ya Kalenga wilayani Iringa, nje kidogo ya Mji wa Iringa.

Dk. Chuwa alisema kumekuwapo na baadhi ya makarani wa sensa ambao wamejijengea utamaduni mbaya wa kupiga picha na kurekodi mahojiano wanayofanya na wahesabiwa na kisha kurusha mitandaoni, akionya kuwa kufanya hivyo ni kosa kwa mujibu wa sheria.

Aliongeza kuwa ni kinyume cha sheria kwa karani yeyote kufanya hivyo anapochukua taarifa za wananchi na waliofanya hivyo, watachukuliwa hatua.

Dk. Chuwa alisema taarifa zinazotolewa na wananchi ni siri, hivyo hazipaswi kurekodiwa wala kupigwa picha.

Alisema tayari wameanza kuwachukulia hatua baadhi ya makarani waliofanya hivyo, akikumbusha adhabu iliyopo kisheria ya faina na kifungo jela.

Pia alibainisha sensa inaendelea vizuri mkoani Iringa, kukishuhudiwa ufanisi mkubwa na kuwa mpaka sasa asilimia 80 ya watu wote mkoani humo wamehesabiwa. Sensa ya Watu na Makazi ni utaratibu wa kukusanya, kuchambua, kutathmini na kuchapisha na kusambaza takwimu za kidemographia, kiuchumi na kijamii kuhusiana na watu wote na makazi yao katika nchi kwa kipindi maalum.

Ni kazi maalum yenye lengo la kupata idadi ya watu wote katika nchi, kwa umri na jinsia, mahali wanapoishi na hali yao ya elimu, hali ya ajira, hali ya vizazi na vifo na hali ya makazi.

Takwimu hizo za msingi ndizo zinazoainisha mahitaji halisi ya wananchi yakiwamo makundi maalum yenye uhitaji maalum kwa mfano, watu wenye ulemavu, wanawake, watoto, vijana na wazee, hivyo kurahisisha uandaaji wa sera na mipango ya maendeleo kulingana na uhitaji na mazingira yaliyoko.


**KUPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA**



117016402

Ndugu **OMAR ABEID MWINDAD** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE175489** iliyotolewa na idara ya Uhamiaji Tanzania. Ilipotea akiwa safarini kutoka Bukoba, kupitia Mwanza kwenda Dar-Es-Salaam. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/336499/2022.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba **0713-752731 au 0754752731.**



**MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA MAGARI CHAKAVU**

i. Wananchi wote mnatangaziawa kwamba Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ikishirikiana na Ofisi ya Msimamizi Mkuu wa Mali za Serikali Mkoa wa Dar es Salaam itaondosha kwa njia ya mnadawa hadhara Magari Chakavu yaliyoko Ofisi za TASAF - Dare es Salaam siku ya Jumatano tarehe 7/09/2022.

ii. Magari yatakayouzwa ni kama ifuatavyo:-

| Na | Aina ya Gari | Idadi |
|---|---|---|
| 1 | Land Rover Defender 110 | 61 |
| 2 | Suzuki Grand Vitara | 1 |

iii. Masharti ya Mnada:-

a) Magari yatauzwa kama yalivyo.

b) Mnunuzi atatakiwa kulipia asilimia 25% ya bei aliyoshinda mara tu baada ya dalali kumtangaza mshindi na kiasi kinachobaki kilipwe katika kipindi cha siku 14 kutoka tarehe ya mnada, Ikiwa mnunuzi atashindwa kulipa kiasi fedha iliyobaki, kiasi alicholipa awali hakitarudishwa.

c) Mtu yeyote atakae tamka bei ya juu kisha akashindwa kulipa asilimia ishirini na tano(25%) ya bei aliyotamka atachukuliwa kuwa ni mwenye kutaka kuvuruga Mnada na hivyo hatua kali zakisheria zitachukuliwa juu yake kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

d) Mnunuzi atatakiwa kuondoa /kuchukua gari alilonunua ndani ya siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.

e) Gharama za kubadilisha umiliki ni jukumu la mnunuzi na atatakiwa kukamilisha taratibu za kumilikishwa kwa mujibu wa sheria ndani ya siku ishirini na moja (21).

f) Wanaopenda kuona magari hayo wataruhusiwa kufanya hivyo siku mbili (2) kabla ya mnada.

g) Mnada utaanza saa nne (04:00) kamili katika maeneyo ya Ofisi za TASAF Dare es Salaam.

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii – TASAF**
**Barabara ya Jakaya Mrisho Kikwete**
**S. L. P. 2719 Dodoma, Tanzania**
**Simu: 255 026 2963866**
**Nukushi: 255 026 2963871**
**Barua pepe: info@tasaf.go.tz**
**Tofuti: www.tasaf.go.tzg**

217010302

# Saba mbaroni tuhuma wizi vifaa nyumba ya watumishi

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

WATUMISHI watatu wa Halmashauri ya Nyang'hwale na wananchi wanne wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Geita kwa tuhuma za wizi wa mabati 60 na maboksi 20 ya marumaru kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa nyumba tatu za watumishi.

Akizungumza mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale, Mkuu wa Wilaya hiyo, Jamhuri Wiliam, alisema kuna miradi ambayo utekelezaji wake ulikuwa ukisuasua, jambo linalozua shaka.

Alisema shida waliyobaini ni udokozi wa vifaa vya ujenzi kwenye miradi ambao unafanywa na watumishi kwa kushirikiana na wananchi wengine wasio waaminifu.

Alisema: "Sasa hivi tunapoongea, tuna watumishi watatu na wananchi wanne ambao wako katika kituo cha polisi ambao tumewakamata na vifaa vya ujenzi mabati 60 pamoja na maboksi 20 ya marumaru.

"Kwa sasa hiyo imetupa taarifa kwamba wizi ulikuwa ukifanyika bila sisi kujua au vyovyote vile, lakini tuanzie hapo, tunafanya uchunguzi wa kina sana ili tuweze kukamata mtandao mzima wa wizi wa vifaa vya ujenzi na watakaobainika, watachukuliwa hatua kali zinazostahili kwa mujibu wa sheria."

William ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wilayani humo, alisema gharama za vifaa hivyo vya ujenzi hazijajulikana kwa sababu polisi wanaendelea na uchunguzi na watuhumiwa wengine wanatafutwa na kwamba upelelezi ukikamilika watafikisha mahakamani.

Alisema polisi wanaendelea na uchunguzi na kwamba wilayani humo kuna ujenzi wa nyumba tatu za watumishi na serikali ilishatoa Sh. milioni 300.




Mkurugenzi wa Huduma za Uchukuzi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Aron Kisaka, akizungumza wakati wa kufungua mkutano wa 12 wa umoja wa vyama vya wahandisi wa mitambo ya kuongozea ndege Afrika (IFATSEA), unaofanyika ijini Dar es Salaam kuanzia Agosti 25 hadi 28 mwaka huu. Mhandisi Aron Kisaka alifungua mkutano huo kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Gabriel Migile. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kuja na bei elekezi kuuza mifugo

**Na Mbaraka Kambona,** GEITA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema serikali iko katika mchakato wa kushirikisha wadau wa sekta ya mifugo kupanga bei elekezi za kuuza mifugo katika minada ili kuwawezesha wafugaji na wafanyabiashara kuuza mifugo yao kwa bei ambayo watakuwa wameshiriki kuipanga.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipotembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa mnada wa kimataifa wa Buzirayombo unaojengwa wilayani Chato mkoani Geita.

Alisema suala la kuwa na bei elekezi serikali inalifanyia kazi na tayari wataalamu walishaandaa na hatua iliyopo sasa ni ya kushirikisha wafugaji na wafanyabiashara wa mifugo ili kwa pamoja wakubaliane na kuja na bei ambayo itakuwa imeridhiwa na pande zote.

"Bei elekezi ikitoka ndiyo itakuwa mahali pa kuanzia na kwenda juu, hivyo tunalifanyia kazi suala hilo na muda siyo mrefu tutatoa mwelekeo wa jambo hilo," alisema.

Waziri huyo aliongeza kwa kuwa sambamba na bei elekezi, serikali inataka mifugo yote nchini ianze kupimwa kwa kilo kama inavyofanyika sasa katika mnada huo wa kisasa wa Buzirayombo.

"Minada yetu yote tutakayoizindua safari hii tunataka iwe na mizani ya kupimia uzito wa mifugo na hili tunataka lifanyike pia katika minada yote ya awali inayomilikiwa na halmashauri zetu nchini ili tuondokane na vitendo vya kuwapunja wafugaji wetu," alifafanua.

Mbunge wa Chato, Dk. Medard Kalemani, aliishukuru serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kujenga mnada huo wa kimataifa wilayani, akiomba kuhakikisha mradi huo unamalizika haraka ili wananchi wa Kanda ya Ziwa na maeneo mengine waanze kuona matunda yake.

# Stanbic, NEEC zaungana kuleta maendeleo kwa wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Stanbic Tanzania imesaini mkataba wa makubaliano na Baraza la Taifa la Uwezeshaji (NEEC) ambao unalenga kujenga ushirikiano baina ya taasisi hizo ili kuendeleza wajasiriamali nchini.

Taasisi hizo zitaunganisha ujuzi, utaalamu, teknolojia na rasilimali zao kutoa mafunzo ambayo yatawawezesha wajasiriamali wa ndani kutumia fursa za uwekezaji nchini na kuongeza ushindani wao wa kikanda na ulimwengu kwa ujumla.

Makubaliano hayo yalitiwa saini na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Stanbic, Kevin Wingfield na Katibu Mtendaji wa NEEC Beng'i Issa, huku yakishuhudiwa na Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega.

Taasisi hizo zitashirikiana kutekeleza programu ya kuwajengea uwezo wajasiriamali iitwayo 'Supplier Development Program' ambayo itawawezesha wafanyabiashara wadogo na wa kati kuboresha biashara zao, pamoja na kutumia fursa, ikiwamo mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (East African Crude Oil Pipeline (EACOP).

Programu hii inatumia mwongozo kutoka Standard Bank Group uliothibitika baada ya kupata mafanikio makubwa nchini Uganda na Msumbiji.

Ulega, alizipongeza taasisi zote mbili kwa kuchukua hatua hiyo ya kusaidia wajasiriamali wadogo na wa kati nchini. Akibainisha kuwa mafunzo hayo ndiyo Watanzania wanayohitaji ili waweze kushiriki na kushindania tenda mbalimbali za miradi ya maendeleo nchini.

Akizungumzia ushirikiano huo, Wingfield alibainisha kuwa Stanbic inazingatia maendeleo ya sekta ya wajasiriamali. "Leo ni mwanzo mpya! Benki yetu kwa kushirikiana na wenzetu NEEC tutatoa mafunzo yatakayowawezesha wajasiriamali wa kitanzania kujijengea na kuongeza uwezo wa kuingia kwenye soko la ushindani na kutumia fursa zilizopo katika miradi mikubwa ya kimkakati nchini. Ninaamini programu hii itafanya mapinduzi ya wajasiriamali na nchi kwa ujumla," alisema.

Kwa upande mwingine, Beng'i alisema, "Ushirikiano wetu na Stanbic utatoa fursa kwa wajasiriamali kupata ujuzi katika Uongozi, Fedha na Hesabu, Kodi, Sheria, Mikataba, Masoko na Manunuzi." Aidha alibainisha kuwa mafunzo hayo yanalenga kujumuisha mikoa sita, lakini yataanzia Dar es Salaam na washiriki 50 watapatiwa mafunzo kwa muda wa miezi mitatu.

Alisema benki hiyo inaamini kwamba ushirikiano ni nguzo muhimu katika safari ya kuunga mkono juhudi za kulenda maendeleo katika sekta ya wajasiriamali na pia kuunda mfumo wa kupanua utaalamu wa benki ili kutoa na kuchochea ukuaji jumuishi na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi.

# Uhaba damu watajwa kuwaathiri wajawazito

**Na Rose Jacob,** MWANZA

ASILIMIA 45 ya wajawazito mkoani Mwanza wanapoteza maisha kutokana na kuchelewa kuongezwa damu wanapofanyiwa upasuaji na kujifungua kawaida.

Kutokana na hali hiyo, wakazi wa mkoa huo wametakiwa kujenga utaratibu wa kuchangia damu mara kwa mara ili kuokoa maisha ya wajawazito, watoto na watu wanaopata ajali.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Thomas Rutachunzibwa, alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa kampeni ya siku ya kuchangia damu duniani.

Katika siku hiyo waumini wa madhehebu ya Kishia kupitia Taasisi ya How is Hussein, walishiriki kwa kujitolea damu ili kusaidia kuokoa maisha ya wengine.

"Kwa Mkoa wa Mwanza ni asilimia 45 ya kinamama wajawazito wanapoteza maisha kutokana na upungufu wa damu, hii imekuwa ni tatizo linalotokana na jamii kushindwa kujitoa kuchangia damu mara kwa mara.

"Wapo watu wanasubiri mpaka wapate shida kwa ndugu zao ndipo wanajitolea damu. Hii ni hatari maana unapotoa damu muda huo, usidhani mgonjwa ataongezwa muda huo huo, ni lazima utaratibu wa kuipima ufanyike ndipo awekewe mgonjwa," alisema.

Dk. Rutachunzibwa alibainisha kuwa mkoa huo una uhitaji mkubwa wa damu na lengo la mwaka huu wa fedha ni kukusanya chupa 49,000 na tangu Julai hadi sasa chupa 3,000 zimeishakusanywa.

Aliongeza kuwa kuna timu 11 za kufanya shughuli ya ukusanyaji wa damu zilizopo kwenye halmashauri zote za mkoa huo katika Hospitali za Bugando, Sekou Toure na kituo cha damu salama cha Kanda ya Ziwa.

"Katika hospitali zetu kubwa za kanda, kuna uhitaji mkubwa mno wa damu kutokana na kufanya upasuaji kwa wagonjwa ambao ni wajawazito, watoto, watu waliopata ajali za bodaboda na magari na ili kuhakikisha adha hii inapata ufumbuzi, kila mwezi kutakuwa na tukio la utoaji damu," alisema Dk. Rutachunzibwa.

Baadhi ya wananchi waliojitokeza kuchangia damu, waliomba serikali kuondoa urasimu wa upatikanaji wa damu pindi mgonjwa wao anapohitaji, wakisisitiza urasmi huo ndiyo sababu ya watu wengi kurudi nyuma linapokuja suala la kuchangia damu.

Dk. Rutachunzibwa alikemea suala la urasimu huku akisema kama damu ipo, hakuna sababu ya kuhangaisha wagonjwa.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha mwananchi anapohitaji damu, anapatiwa na njia ya kupata damu kwa wingi ni kuhamasisha jamii kujitokeza kuchangia kwa hiari.

Mwenyekiti wa Taasisi ya How is Hussen Mkoa wa Mwanza, Mohamed Moledina, alisema jumuiya ya vijana na wanawake wa Kiislamu imechukua jukumu la kuhamasisha suala la upatikanaji wa damu salama kwa jamii nzima.

"Lengo la taasisi yetu ni kukusanya damu uniti 50,000 kwa dunia nzima. Leo tumefanya shughuli hii kidunia nzima na hapa Mwanza tumekusanya uniti zaidi ya 110.

"Tunaomba jamii tuhamasishane kutoa damu kabla ya mgonjwa hajahitaji na hii itasaidia sana, siyo vyema kutoa damu muda huo huo kisha apewe mgonjwa," alisema Moledina.

Alisema mwitikio ulikuwa mkubwa kwa makundi mbalimbali wakiwamo madereva wa pikipiki, maarufu bodaboda, wananchi wa kawaida, viongozi wa dini na viongozi wa matawi wa Klabu ya Simba jijini Mwanza.




Mkuu wa Mauzo wa Kanda ya Dar es Salaam na Pwani Vodacom Tanzania PLC, Brigita Shirima (kulia), akimkabidhi funguo mshindi wa bajaj wa promosheni ya M-Pesa Imeitika kutoka Kimara jijini Dar es Salaam, Magdalena Magoma Moke, katika hafla ya kukabidhi bajaj moja na bodaboda tano kwa washindi wa awamu ya sita iliyofanyika viwanja vya Barafu Mburahati jijini humo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Askari wanusurika kifo uvamizi wa wananchi

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

ASKARI watatu wa maliasili wamenusurika kifo baada ya kuvamiwa na kushambuliwa kwa silaha za jadi yakiwamo mapanga na marungu na wananchi wa Kijiji cha Butengo, Kata ya Butengolumasa wilayani Chato mkoani Geita, kwa madai ya kuingia kwenye mashamba yao.

Mkasa huo ulitokea juzi mchana katika kijiji hicho baada ya askari hao kuonekana katika shamba la serikali la Silayo wakipanda miti.

Baada ya mkasa huo wa kuvamiwa askari hao, walijitahidi kujiokoa kwa kukimbia lakini walizidiwa na kundi la wananchi hao na kujikuta wakipigwa na kujeruhiwa katika maeneo mbalimbali ya miili yao.

Mmoja wa askari hao waliovamiwa na wananchi, Hendry Mollel, akisimulia kilichojiri dhidi yao akiwa katika Hospitali ya Waja mkoani Geita alikolazwa kwa ajili ya matibabu, alisema kuwa Agosti 26 majira ya saa 7:30 mchana, akiwa na wenzake, walivamiwa na wananchi wakiwa katika shamba lao wakipanda miti kwa msimu wa mwaka huu.

Alisema wakiwa wanaendelea na kazi zao, ghafla lilitokea kundi la watu zaidi ya 30 wakiwa na silaha za jadi, yakiwamo marungu na mapanga na kisha kuanza kuwashambulia wakiwatuhumu kuvamia maeneo yao waliyopewa na serikali.

Askari huyo alisema kuwa kundi la watu hao lilitokea eneo la njia ya panda ya Nyakayondwa na Chato na wakati wakijaribu kujiokoa kwa kuwakimbia, mwenzao alipigwa na kuanguka chini kisha watu hao walianza kumshambulia kwa silaha za jadi akiwa chini na kumjeruhi sehemu mbalimbali za mwili.

"Tulijaribu kujiokoa kwa kukimbia kwa kuwa hatukuwa na silaha yoyote, ghafla tukajikuta tumezingirwa licha ya kujitahidi kuwapa elimu tukiwaeleza kuwa kama wamepewa maeneo hayo na serikali, wafuate utaratibu, sisi kazi yetu ni kusimamia shamba la miti na kupanda miti kwenye maeneo ambayo mazingira yameharibiwa, hawakutuelewa, mimi nilipigwa mgongoni na mguu wa kushoto," alisimulia Mollel.

Mhifadhi Msaidizi, Rehema Shomve, alisema kuwa baada kundi hilo kuanza kuwashambulia, alipigwa na kudondoka chini na kisha watu hao kuanza kumshambulia kwa silaha za jadi huku akipiga kelele kuomba msaada.

"Kwa kweli nina maumivu makali, nimepigwa na kujeruhiwa mgongoni, mkononi, mguu wa kulia kama mnavyoniona, nilisaidiwa na wasamaria wema waliokuwa wakitoka shambani, wenzangu walifanikiwa kukimbia, mimi nikaanguka chini ila ninamshukuru Mungu niko hai," alisema Rehema.

Mhifadhi Mkuu wa Shamba hilo, Juma Mseti, akiwa hospitalini hapo, alisema alipata taarifa ya askari hao kushambuliwa na kundi la watu hao wakati akiwa Buchosa kwenye ziara ya Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii baada ya kupigiwa simu.

Alisema kuwa baada ya kupokea taarifa hizo, aliwasiliana na askari wa Kituo cha Polisi Bwanga kwa ajili ya kuomba msaada.

Baada ya askari hao kupata taarifa hiyo, walikwenda eneo la tukio na kuwaokoa majeruhi na kuwakimbiza Kituo cha Afya Bwanga wilayani Chato kwa ajili ya kupewa huduma ya kwanza.

Mseti alisema kuwa baada ya kupewa huduma ya kwanza, askari hao walipewa rufani kwenda Hospitali ya Waja wilayani Geita kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Aliwataja askari wake waliovamiwa kuwa ni Molleli, Rehema na Wilfred Samuel.

Mhifadhi huyo alisema shamba hilo lilizinduliwa mwezi Januari, 2021 na Rais wa awamu ya tano, Hayati Dk. John Magufuli na lina ukubwa wa hekta 69,756.

Shamba hilo linasimamiwa na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kwa kupanda miti na kudhibiti uharibifu wa mazingira ndani ya hifadhi.

"Sisi TFS tunalaani kitendo cha askari wetu kupigwa na kujeruhiwa wakati wakiwa katika majukumu yao," alisema Mseti.

Mganga Mkuu Msaidizi wa Hospitali ya Waja, Dk. Nehemia Kilave, alikiri kuwapokea askari hao majira ya saa moja jioni juzi wakitoka Kituo cha Afya Bwanga wilayani Chato mkoani Geita na kuwapatia huduma.

Mganga huyo alisema kuwa baada ya kuwafanyia uchunguzi wa awali, walibaini kuwa walikuwa wamepata majeraha sehemu za mgongoni, mikononi na miguuni huku mmoja wao (wa kike) akiwa na majeraha zaidi na kwamba wote walitibiwa na kuruhusiwa kurejea nyumbani.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martin Shigella, tayari ameagiza kusakwa na kukamatwa kwa wananchi hao waliofanya ukatili huo ili wafikishwe kwenye vyombo vya sheria.

Shigella alitoa agizo hilo juzi alipowatembela majeruhi hao katika hospitali hiyo na kusema kuwa kama wananchi hao walikuwa na malalamiko, walipaswa kufuata utaratibu.

Alisema vitendo kama hivyo havikubaliki katika mkoa wake na lazima vyombo vya ulinzi na usalama kufanya kazi yao.

# Watoto 360,000 kupewa chanjo

**Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA**

WATOTO 363,315 mkoani Singida wenye umri chini ya miaka mitano, wanatarajia kupewa chanjo ya matone dhidi ya ugonjwa wa polio ili kujikinga na maradhi hayo.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema hayo mjini hapa juzi katika kikao cha uhamasishaji wa kampeni ya utoaji wa chanjo ya matone dhidi ya ugonjwa wa polio.

Serukamba alitoa mchanganuo kuwa katika kazi hiyo Wilaya ya Iramba inatarajiwa kuwafikia watoto wasiopungua 56,360, Wilaya ya Singida watoto 58,197, Manyoni 45,416, Manispaa ya Singida 39,841, Wilaya ya Ikungi 77,638, Wilaya ya Mkalama 51,658 na Itigi 34,205.

Alisisitiza kwamba katika maandalizi hayo wataalamu wa afya wataendesha kazi hiyo katika vituo vya kutolea huduma ya afya na kwa kutumia njia ya mkoba na kampeni hiyo itaendeshwa nyumba kwa nyumba, mtoto kwa mtoto ili kuwafikia wote.

Mkuu wa Mkoa alitoa wito kwa wakuu wa wilaya kupitia kamati za afya ya msingi za halmashauri kusimamia utoaji wa huduma ya chanjo kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na zitakazotolewa kwa njia ya mkoba ili kuwafikia watoto kwa asilimia 100.

Aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri kuweka mikakati ya kuhakikisha watoto wote waliokosa chanjo ya awamu ya kwanza na pili, wanapata awamu hii.

Serukamba pia alihimiza wananchi kuhakikisha wanajitokeza kushiriki katika kampeni hiyo na kuwapeleka watoto wao kupata chanjo kwa ajili ya maisha yao.

Mratibu wa Chanjo ya Polio Mkoa we Singida, Habibu Mwinorya, alisema kampeni hiyo ilianza jana wakati uchanjaji utaanza Septemba Mosi mwaka huu.

Habibu alisema tayari dozi 350,000 zimekwishasambazwa katika halmashauri zote saba za Mkoa wa Singida na mpaka sasa zimekwishapelekwa katika vituo vyote vya kutolea huduma.

# RC apata mwarobaini kutokomeza umaskini wanufaika TASAF

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, ameagiza wanufaika wa sasa wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) wawe kizazi cha mwisho na pasiwapo na wengine kwa kuwa fursa za kiuchumi zilizopo mkoani humo ni nyingi.

Pia amewaagiza viongozi wa Wilaya ya Ludewa kuwahamasisha wananchi kuwekeza kwenye mazao ya biashara ili yawasaidie uzeeni.

Alitoa agizo hilo jana alipozuru wilayani Ludewa kuhamasisha Sensa ya Watu na Makazi ambayo kwa wilaya hiyo hadi usiku wa Agosti 25, ilikuwa imefanikiwa kwa asilimia 90.

"Ni vizuri tuseme kwamba tutafika kizazi cha mwisho, pengine hawa watu wanaoishi katika umaskini katika mpango wa TASAF, waliopo leo tuseme wazi kitakuwa cha mwisho kwa kuwa tunazo fursa nyingi za uchumi zinazoweza kututoa huko," alisema.

Mtaka alisema anataka kuona kizazi kilichoko sasa kinakuwa na elimu ambayo itakuwa ukombozi kwa upande wao na kuleta mtazamo tofauti utakaolisaidia taifa baadaye.

Pia alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Sanday Deogratias, kuanza kuweka rekodi ya vijana wanaofanya vituko mitaani kwa kuzingatia wasifu wao ili rekodi hiyo itumike uzeeni watakapokwenda kuomba kuingizwa kwenye orodha ya wanufaika wa TASAF.

"Tunataka tuanze kuweka rekodi za vijana wote wanaofanya vituko sasa kwenye ujana wao ili tuje tuitumie uzeeni, mtu akiuza shamba lake au la baba yake tunaweka kwenye rekodi, mtu akigoma kwenda shuleni, tunaweka kwenye rekodi, mtu akifukuzwa kazi kwa sababu ya ulevi, naye tunamweka kwenye rekodi ili akizeeka maskini na akahitaji msaada wa TASAF, tunamwonyesha vituko alivyofanya ujanani," alisema.

Aliwataka wazazi wilayani humo kuhakikisha wanawasomesha watoto wao ili wapate ujuzi ambao utawasaidia kujiajiri na kuajiriwa kwenye kampuni mbalimbali.

Alikumbusha kuwa Ludewa ni wilaya ya kimkakati yenye miradi mikubwa ya Liganga na Mchuchuma ambayo hivi karibuni itaanza utekelezaji wake, hivyo watoto wao wasije kuwa vibarua au kukosa kabisa ajira kutokana na kukosa vigezo vya kielimu.

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Andrea Tsere, alisema wanaendelea na shughuli za uhamasishaji uwekezaji kwa wananchi kwa kurejesha baadhi ya mazao yaliyokuwa hayapewi kipaumbele.

"Ludewa ina ardhi nzuri sana kwa kilimo, mazao mengi ya biashara yanakubali hapa, hivi sasa tupo tunafanya uhamasishaji wa kilimo cha mazao ya biashara na kurejesha baadhi ya mazao yaliyosahaulika, mfano korosho.

"Kwasasa hapa Ludewa kwa mwaka tunavuna tani 150, lakini tumeleta zao la parachichi, awali huku walikuwa wanalima miti ya mbao tu," alisema Tsere.

Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga, alisema serikali imetenga Sh. bilioni 16 kwa ajili ya ulipaji wa fidia kwa watu waliopisha maeneo yao kutokana na mradi wa Mchuchuma na Liganga.

Aliwataka wananchi kufanya uwekezaji kwenye nyanja zote za kiuchumi ili miradi hiyo itakapofunguliwa, wawe na njia nyingi za kujiongezea kipato na kujikimu kimaisha.



Wafanyakazi wa Kampuni ya GF Trucks & Equipments Ltd wakishiriki uchangiaji damu kwa hiari wakati wa kambi ya matibabu bure ya maradhi yasioambukiza iliyoandaliwa na Jumuiya ya Kiislamu ya Khoja Shia Ithnasheri, kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi waondokana na kero upatikanaji maji

**Na Joseph Mwendapole**

UGUMU katika upatikanaji wa maji kwa wakazi wa Mtaa wa Kibesa, Kata ya Mabwepande na Mpiji Magohe, Wilaya Kinondoni, Dar es Salaam umetatuliwa baada ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira (DAWASA) kukamilisha mradi wa maji Kibesa.

Wakazi wa eneo hilo walikuwa wakilazimika kutumia muda mwingi kutafuta maji visimani na hata kutumia fedha nyingi kununua maji ya mitaani ambayo hayana uhakika wa usalama kiafya.

Akizungumzia hali ya huduma ya maji, Mwenyekiti wa Mtaa wa Kibesa, Said Diuchile, alisema jana kuwa kwa sasa wanaridhishwa na upatikanaji wa maji mtaani kwao na kuwataka wananchi kuendelea kujitokeza kuunganishiwa maji.

"Tulifanya mikutano na DAWASA na walituahidi ifikapo mwezi wa nane (Agosti) tutapata huduma, niwashukuru kwa kutekeleza hilo kwa kuwa sasa tunapata majisafi.

"Tulihitaji huduma hii, sasa hata shughuli za maendeleo zitakwenda kwa kasi, ni wakati wetu sasa tujitokeze kuunganishiwa huduma ya maji ili yafike kwenye nyumba zetu," alisema Diuchile.

Mkazi wa Mtaa huo, Catherine Challe, alisema kwa muda mrefu walikuwa na keri katika kupata majisafi na salama, hivyo ujio wa mradi huo ni ukombozi kwao.

"Kila mtu anajua huduma ya maji katika eneo letu ilikuwa ni ndoto, zilianza kama habari tu na wengi hatukuamini kwamba iko siku tutapata maji ila DAWASA wametekeleza mradi huu na sasa tunapata majisafi, tunawapongeza sana na kuahidi kutoa ushirikiano katika ulipaji wa huduma hizi," alisema Catherine.

Msimamizi wa mradi huo kutoka DAWASA Mabwepande, Juma Kalemera, alisema kwa sasa wananchi wengi wanajitokeza kuunganishiwa huduma ya maji.

"Tumeanza kuunganisha huduma ya maji kwenye mradi huu wa maji Kibesa ambao chanzo chake ni tangi la Malolo lenye ujazo wa lita milioni sita, matarajio yetu ni kupata zaidi ya wateja 1,600 katika eneo la Mabwepande (Kibesa) na Mpiji Magohe, ambako mpaka sasa zaidi ya wateja 100 wameunganishwa," alisema Kalemera.

Nipashe
Spotika




NYOTA 10 WATAKAOCHEZA KOMBE LA DUNIA 2022 LA MWISHO KWAO UK. 12




# KWA NINI CASEMIRO USAJILI MZURI MANCHESTER UNITED?

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United hatimaye imemsajili kiungo, Casemiro kutoka Real Madrid. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alijiunga na 'Mashetani Wekundu' hao baada ya kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu na taratibu nyingine na pia alishuhudia mchezo wa klabu hiyo dhidi ya Liverpool Jumatatu usiku, ambao waliibuka na ushindi wa mabao 2-1.

Washindi hao mara 13 wa Ligi Kuu England, walionekana kuwa na heshima katika mechi zao za kabla ya msimu mpya chini ya kocha mpya, Erik Ten Hag, lakini walikumbwa na hali mbaya katika mechi zao mbili za kwanza za msimu huu.

Ukosefu wa kiungo wa kati wa safu ya ulinzi umedhihirika katika misimu miwili iliyopita na huenda Man United sasa wamesajili mmoja wa wachezaji bora zaidi kwenye idara hiyo.

Ingawa kuna wengi wanaohoji kuwa pauni milioni 70 kwa raia huyo kutoka bara la Amerika Kusini kuwa ni nyingi mno, kuna kila sababu ya mashabiki wa klabu hiyo kufurahia ununuzi huu.

Katika kulifafanua hilo, hebu tuangalie sababu tatu zinazomfanya Casemiro awe usajili mzuri wa Man United...

**#3. Husaidia haraka nafasi ya ulinzi**

Manchester United imekuwa ikimlilia kiungo mkabaji tangu utawala wa Ole Gunnar Solskjaer katika klabu hiyo. Kocha huyo wa Norway labda angefurahia kusajiliwa kwa kiungo wa kati msimu uliopita badala ya kumnunua Cristiano Ronaldo.

Pia inaeleweka kwa nini Ten Hag amekuwa akisisitiza kuhusu klabu hiyo kumnunua Frenkie de Jong tangu siku ya kwanza kuwa hapo Man United. Ingawa klabu imefanya kila wawezalo katika hilo, hadi sasa limeshindwa kutekelezwa.

Kwa Casemiro, 'Mashetani Wekundu' hao wamemnyakua kiungo bora zaidi wa ulinzi katika soka la dunia ya hivi sasa. Ingawa alifikisha miaka 30 mwaka huu, Mbrazil huyo alikuwa bora kwa Real Madrid katika ushindi wao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu uliopita.

Ili kutoa mwanga zaidi kuhusu hilo, kiungo huyo alishika nafasi ya kwanza kwa asilimia 40 ya presha iliyofanikiwa katika LaLiga msimu uliopita. Pia alikuwa miongoni mwa wachezaji watano bora waliookoa hatari nyingi zaidi kwa kukaba (mara 64) kwenye ligi.

Kwa hiyo, kiungo huyo asiyetaka ujinga kazini, anaweza kulinda safu ya nyuma ya Man United na kutoa uti wa mgongo unaohitajika kwa kikosi cha Ten Hag.

Uimara wake wa ulinzi unaweza pia kurudisha imani kwa Harry Maguire na Lisandro Martinez na kuwafanya wahisi kuwa na uhakika zaidi. Vile vile, mstari wa mbele utakuwa na uhuru zaidi wa kushambulia na kufanya idadi zaidi kwenda mbele, na hivyo kuwaruhusu kuongeza uwezo wao wa kusaka bao.

Kuongezwa kwake kunaweza kuinua kiwango cha uchezaji wa wachezaji kadhaa wa timu kwani anaweza kuwa mchezaji bora katika nafasi ambayo walihitaji kuijaza kwa muda mrefu.

**#2. Morali ya ushindi**

Jambo moja ambalo linaweza kusemwa kwa wachezaji wengi wa Real Madrid wa muongo mmoja uliopita ni ari na morali yao ya kushinda na kutokata tamaa.

Hakika Casemiro ni mmoja wao na tabia yake hiyo inaweza kuwa chachu kubwa kwa wachezaji wa Man United. Huku Ronaldo na Raphael Varane wakitokea klabu moja, Mbrazil huyo anaweza kuongeza kitu kipya hapo.

Uwezo wa kushikilia katika michezo mikali na kupata matokeo ukiwa ndio akili na hasira ya kushinda ni moja ya tabia ya Casemiro. Aidha, ataisukuma klabu hiyo kuendelea na kuwania mataji msimu huu, bila kujali ukubwa wa mashindano.

Kuongezwa kwake kunaweza pia kuifanya klabu kuwa ya vitendo zaidi katika michezo mikubwa, kwa sababu tu ya uzoefu wa mchezaji kucheza katika mechi kama hizo.

Casemiro, ambaye ameshinda mataji matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, mataji matatu ya Klabu Bingwa Dunia, mataji matatu ya LaLiga, na mataji matatu ya UEFA Super Cup, anajua nini kinahitajika ili kushinda taji.

Atakuwa na hamu ya kuingiza akili hiyo katika kikosi cha sasa cha Man United, jambo ambalo wamekosa kwa zaidi ya muongo mmoja sasa.

**#1. Kiongozi ambaye Man United ilimhitaji**

Tabia moja ambayo Man United imekuwa ikikosa sana miaka ya hivi karibuni ni ya kiongozi. Ingawa Ronaldo hakika anajaribu kuongoza kutoka mbele, lakini hawezi kuongoza timu nzima. (Pia anaripotiwa kutaka kuondoka klabuni hapo.)

Hata hivyo, hilo haliwezi kusemwa kwa Casemiro, ambaye atakuwa sauti kubwa kila mara katikati ya uwanja kwa Man United. Mbrazil huyo ana sauti kubwa katika safu ya kiungo na atadai asilimia 100 kutoka kwa Fred na Scott McTominay, ambao hawapo kwenye kiwango bora katika miezi 18 iliyopita.

Zaidi ya hayo, kiungo huyo mkabaji anatoka katika kikosi cha Real Madrid ambacho kimekuwa kikitengeneza wachezaji wa kucheza kwa moyo mmoja.

Shauku yake, nguvu, na uwezo wa kufanya kazi kwa kiwango cha juu hadi dakika ya mwisho ni hakika kuwatawanya wachezaji wenzake wapya.

Man United kwa sasa wanapitia kipindi kibaya zaidi katika historia ya Ligi Kuu England. Kwa hivyo, kiongozi kama Casemiro anaweza kubadilisha mambo kuwa bora, na hivyo kumfanya kuwa mchezaji bora zaidi wa klabu katika miaka ya hivi karibuni.

## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, kwa sasa ndiye anayeshikilia rekodi ya kufunga mabao mengi kwa klabu moja kwenye Ligi Kuu England baada ya kutupia mara 185 katika mechi 285, akimpiku nyota wa zamani wa Man City, Sergio Agüero, ambaye alifunga mabao 184 katika mechi 275. Mabao hayo ya Kane ni kabla ya mchezo wao wa jana dhidi ya Nottingham Forest.






# NYOTA 10 WATAKAOCHEZA KOMBE LA DUNIA 2022 LA MWISHO KWAO

**LONDON, England**

KOMBE la Dunia la FIFA la 2022 liko karibu kabisa. Tumebakiza miezi miwili kabla ya mchezo wa ufunguzi wa mashindano hayo makubwa zaidi yanayofanyika kila baada ya miaka minne kuanza. Kombe la Dunia bila shaka ni tukio kubwa zaidi la soka duniani na ni ndoto ya kila mchezaji kuwakilisha taifa lake.

Ni timu bora pekee duniani ambazo zimefuzu kwa Kombe la Dunia. Tutazikosa timu bora kama Italia, Colombia, Sweden, Chile na Nigeria, ukizitaja kwa uchache ambazo zimeshindwa kufuzu.

Baadhi ya nyota wakubwa wa soka kama Erling Haaland, Mohamed Salah, Marco Verratti na David Alaba, ni miongoni ambao hawatashiriki Kombe la Dunia la 2022 baada ya timu zao za taifa kushindwa kufuzu.

Kombe la Dunia la 2022, ambalo litafanyika nchini Qatar, pia huenda likawa mara ya mwisho kuwaona baadhi ya wachezaji wakubwa wanaotawala soka la kisasa duniani.

Hapa tunawaangalia wanasoka nyota 10 ambao michuano hii inaweza kuwa ya mwisho kwao kuzichezea nchi zao, haya sasa...

**#10. Edinson Cavani (Uruguay)**

Edinson Cavani ni mmoja wa washambuliaji bora wa kizazi chake. Mchezaji huyu wa kimataifa wa Uruguay, amefunga mabao 56 na kutoa pasi za mabao 17 katika mechi 129 alizocheza hadi sasa katika timu yake ya taifa. Cavani anafahamika kwa uwezo wake wa kumalizia na kuongoza vizuri, pia anasifika kwa ukakamavu wake na ari yake ya kuipigania nchi yake.

Ana umri wa miaka 35 sasa na Kombe la Dunia la FIFA la 2022 huenda likawa la mwisho kwake. Cavani, ambaye aliondoka Manchester United baada ya mkataba wake kumalizika mapema msimu huu wa majira ya joto, kwa sasa ni mchezaji huru.

**#9. Luis Suarez (Uruguay)**

Mshambuliaji patina wa Cavani, Luis Suarez pia ni mchezaji bora wa kisasa. Suarez pia ana umri wa miaka 35 na kwa sasa anaitumikia klabu ya Nacional ya nchini Uruguay. Yeye ni mmoja wa washambuliaji wazuri zaidi wa zama za kisasa na amewatia hofu mabeki wengi wa Ulaya akiwa katika ubora wake.

Suarez amepita miaka yake ya kilele sasa na kiwango chake kimeshuka katika misimu ya hivi karibuni. Kwa hiyo, Kombe la Dunia la FIFA la 2022 huenda likawa la mwisho kwa El Pistolero huyo.

**#8. Angel Di Maria (Argentina)**

Angel Di Maria amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi wa Argentina katika muongo mmoja uliopita. Kutokuwapo kwake kutokana na jeraha kunatajwa na wengi kama sababu kuu iliyoifanya Argentina kushindwa kuifunga Ujerumani katika fainali ya Kombe la Dunia la FIFA la 2014.

Di Maria alifunga bao la ushindi la La Albiceleste hao katika fainali ya 2021 ya Copa America. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alijiunga na Juventus kama mchezaji huru mapema msimu huu wa majira ya joto na ingawa hayuko kwenye kilele cha uwezo wake, bado ni mwanasoka mzuri sana.

Lakini hakuna uwezekano wa kuwapo kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2026.

**#7. Marco Reus (Ujerumani)**

Marco Reus bila shaka ni mmoja wa washambuliaji bora wa kizazi chake. Kwa bahati mbaya, ushiriki wake katika timu ya Taifa ya Ujerumani umekuwa mdogo kutokana na majeraha. Ameichezea mara 48 pekee katika maisha yake ya soka, akifunga mabao 15 na kutoa pasi 14 za mabao.

Reus amecheza mechi tatu pekee kwenye Kombe la Dunia na atakuwa na matumaini ya kushiriki kwa kiasi kikubwa wakati huu. Hii inaweza kuwa nafasi ya mwisho ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, kucheza katika mashindano hayo.

**#6. Thiago Silva (Brazil)**

Brazil haina upungufu wa walinzi wa kiwango cha kimataifa kuelekea Kombe la Dunia la FIFA 2022. Beki huyo wa kati wa Chelsea mwenye umri wa miaka 37, atakuwa mtu wao mkuu katika safu ya tatu ya ulinzi. Mkongwe wa mchezo huo, Silva bado ni 'mnyama' kabisa nyuma ingawa anakaribia miaka 40. Huenda hili likawa Kombe la Dunia la mwisho la Silva na Brazil.

#5. Thomas Muller (Ujerumani)

Thomas Muller ni nyota kwa kikosi cha Ujerumani. 'Mfalme wa asisti' wa Ulaya ni mmoja wa wanasoka wenye kipaaji cha kiufundi na akili kwenye sayari hii. Fowadi huyo wa Bayern Munich anaendelea kufanya kazi kwa kiwango cha juu licha ya kuwa amebakisha wiki chache tu afikishe umri wa miaka 33.

Katika mechi 16 za Kombe la Dunia kwa Ujerumani, Muller amefunga mabao 10 na kutoa asisti sita. Namba hizi ni ushahidi wa jinsi mshambuliaji huyo mkongwe alivyo muhimu kwa timu ya Taifa ya Ujerumani.

**#4. Karim Benzema (Ufaransa)**

Karim Benzema alirudishwa katika timu ya Taifa ya Ufaransa mwaka 2021 baada ya kukosekana kwa miaka sita. Mfaransa huyo amekuwa katika kiwango cha hali ya juu katika klabu ya Real Madrid hivi karibuni na mambo makubwa yanatarajiwa kutoka kwake kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022.

Hata hivyo, Benzema ana umri wa miaka 34 sasa na huenda hii ikawa mara yake ya mwisho kucheza Kombe la Dunia. Ni mmoja wa washambuliaji walio katika kiwango bora zaidi duniani na anaweza kuwa nyota muhimu zaidi kwa mafanikio ya Ufaransa.

**#3. Luka Modric (Croatia)**

Luka Modric alishinda Mpira wa Dhahabu, tuzo kwa mchezaji bora wa mashindano, katika Kombe la Dunia la FIFA la 2018. Aliiongoza Croatia kutinga fainali miaka minne iliyopita, ambapo hatimaye walipoteza kwa Ufaransa. Modric atakuwa na umri wa miaka 37 wakati Kombe la Dunia la FIFA 2022 linaanza.

Hata hivyo, amekuwa katika kiwango cha hali ya juu kule Real Madrid hivi karibuni na kwa mara nyingine atakuwa mchezaji mkuu wa Croatia.

**#2. Lionel Messi (Argentina)**

Lionel Messi ndiye mwanasoka bora zaidi wa wakati wote. Mshindi huyo wa tuzo ya Ballon d'Or mara saba amekuwa katika daraja la aina yake katika maisha yake yote. Alitawazwa 'Mchezaji Bora wa Mashindano' kwenye Copa America ya 2021 baada ya kuiongoza Argentina kutwaa taji hilo kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1993.

Messi amefunga mabao 86 na kutoa asisti 51 katika mechi 162 alizoichezea 'La Albiceleste' katika maisha yake ya kimataifa. Kombe la Dunia ndilo taji pekee ambalo halipo kwenye kabati lake la mataji. Michuano hii itakuwa ya mwisho kwake, kwa sababu hivi sasa ana umri wa miaka 35.

**#1. Cristiano Ronaldo (Ureno)**

Cristiano Ronaldo ndiye mfungaji bora wa muda wote katika soka la kimataifa la wanaume. Amefunga mabao 117 na kutoa asisti 42 katika mechi 189 alizoichezea timu ya Taifa ya Ureno. Ronaldo ni mmoja wa wanasoka bora wa wakati wote.

Watu watammisi sana atakapoamua kutundika daluga zake. Ronaldo sasa ana umri wa miaka 37 na hakuna uwezekano wa kuwapo kwenye Kombe la Dunia la FIFA 2026.

## Nukuu


"Alichokifanya leo amekifanya katika maisha yake yote. Si kitu maalum. Ningesema asante kwangu kwa mawazo yangu mahiri, lakini ningesema Erling [Haaland] amefanya hivi tangu alipozaliwa, siku zote amefanya hivi katika maisha yake, akiwa Salzburg, BVB [Borussia Dortmund], kila mara alifunga mabao, ana uwezo wa ajabu wa kufunga mabao, alikuja kwa ajili hiyo," **Kocha Man City, Pep Guardiola baada ya Haaland kufunga hat-trick wakati wakishinda 4-2 dhidi ya Crystal Palace juzi.**



"Mashabiki waendelee kujitokeza kwa wiki uwanjani kutusapoti kwa sababu sisi licha ya kuiwakilisha Simba, tunaliwakilisha pia taifa kwenye mechi za kimataifa, ninaamini huko tunapoenda tutaiwakilisha Simba na taifa na tutafanya vizuri," **Nahodha wa Simba Queens, Fatuma Issa 'Fetty Densa' baada ya kutwaa ubingwa wa Cecafa kwa Wanawake na kukata tiketi ya kuuwakilisha Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.**



"Kama ningekuwa mkurugenzi wa michezo, ningempa [Mohamed Salah], mwaka mmoja ili ajithibitishe. Je, una thamani ya miaka mingine (mitatu)? Anahitaji kutoa namba sawa, hasa kwa mshahara anaolipwa. Nadhani ni muhimu sana kwa Salah, na pia kwa Liverpool, kutafuta njia ya kufanikiwa pamoja ili kujitahidi kubakia Liverpool kwa muda mrefu," **nyota wa zamani wa Uholanzi, Nigel de Jong.**



# MABEKI WA 5 WALIOTUPIA MABAO LIGI KUU 2022/23

Na Adam Fungamwango

LIGI Kuu Tanzania Bara imefikia kwenye raundi ya pili huku jumla ya mabao 40 yakiwa yamefungwa, kila raundi ikiwa na mabao 20. Mabao hayo yamevunja rekodi ya msimu uliopita ambapo yalifungwa 22 kwenye raundi mbili za mwanzo.

Kwenye raundi ya kwanza msimu uliopita yalipachikwa mabao 10 na raundi ya pili yakafungwa 12.

Kati ya mabao hayo 40, matano yamefungwa na mabeki. Pamoja na kwamba timu zimesajili mastraika ambao wana kazi ya kupachika mabao, lakini kwa raundi mbili tu, mabeki nao ambao kazi yao kubwa ni kuzuia wameonekana kuja juu kwenye ufungaji.

Makala haya, yanakuchambulia mabao matano ambayo yamefungwa na mabeki kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

**#1. Vidastus Mwihambi (Mtibwa vs Namungo)**

Anacheza kama beki wa kati kwenye kikosi cha Mtibwa Sugar. Aliweka rekodi ya kuwa beki wa kwanza kufunga bao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu katika mechi ya ufunguzi wa ligi dhidi ya Namungo. Ilichezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Agosti 15, mwaka huu na timu hizo kutoka sare ya mabao 2-2.

Mwihambi anayecheza namba tano, alilifunga bao hilo kwa kichwa dakika ya 54, baada ya kuunganisha mpira wa faulo kutoka kwa Ismail Aidan likiwa ni bao la kusawazisha baada ya kufungwa la kwanza.

**#2. Nickson Kibabage (Mtibwa vs Namungo)**

Ilikuwa ni kama kopi tu ya bao la kwanza lililofungwa na Mtibwa Sugar kwenye mechi dhidi ya Namungo.

Siku hiyo hiyo, Agosti 15, mwaka huu kwenye mechi dhidi ya Namungo, bao la pili la Mtibwa lilifanana sana na la kwanza. Tofauti ilikuwa ndogo sana.

Ilikuwa ni faulo kwenye lango lile la upande wa kusini ikipigwa na yule yule Ismail. Safari hii aliamua kunyoosha, akapiga shuti moja kati lililotemwa na kipa Jonathan Nahimana, beki namba tatu Nickson Kibabage aliyeingia kipindi cha pili, naye alikwenda mbele kuangalia kama anaweza kupata kitu. Baada ya kipa kuutema, aliuwahi haraka na kuukwamisha wavuni dakika ya 79, likiwa ni la pili, kabla ya Namungo kusawazisha baadaye.



Bakari Mwamnyeto

**#3. Bakari Mwamnyeto (Yanga vs Polisi Tanzania)**

Nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto yumo kwenye orodha ya mabeki waliofunga mabao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

Alilifunga Agosti 16, mwaka huu kwenye Uwanja Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, timu yake ikishinda mabao 2-1, ikiwa ni mechi ya kwanza. Lilikuwa ni bao muhimu kwenye mechi hiyo, kwani wakati huo timu hizo zilikuwa sare ya bao 1-1.

Dakika tano kabla ya mechi kumalizika, kona iliyopigwa na Bernard Morrison, ilimkuta beki huyo namba tano akiwa kwenye nafasi nzuri, akiwa hajakabwa na mtu yeyote, huku mabeki wa Polisi Tanzania wakiwa wamejirundika na kujikaba wenyewe, akaukwamisha mpira wavuni, akiandika bao la pili na la ushindi, Yanga ikishinda 2-1.

**#4. Samson Madeleke (Mbeya City vs Dodoma Jiji)**

Madeleke, akicheza namba nne kwenye kikosi cha Mbeya City, Agosti 17, mwaka huu alifunga bao kwa kichwa, akiunganisha mpira wa kona na kuisawazishia timu yake wakati huo ikiwa imeshachapwa bao moja.

Bao hilo la dakika ya 26 lilionekana kuwarudisha mchezoni na kupata mabao mengine yaliyofungwa na Sixtus Sabilo na Elius Ambokile na kuifanya Mbeya City kuibuka na ushindi wa 3-1 ikiwa ugenini, Uwanja wa Liti mkoani Singida.

**#5. Chilo Mkama (Polisi Tanzania vs KMC)**

Mkama ni beki wa kati wa Polisi Tanzania ambaye naye yumo kwenye orodha ya mabeki waliofunga mpaka sasa.

Beki huyu wa zamani wa Geita Gold, aliufuma mpira wa kona uliokuwa unazagaazagaa langoni mwa KMC, akaujaza wavuni, mechi ikichezwa Agosti 21, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Kwenye mechi hiyo, timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2, na hilo lilikuwa ni bao la pili, kabla ya KMC kusawazisha kwa mkwaju wa penalti na Matheo Antony, nyota wa zamani wa Yanga, aliyefunga mabao yote mawili kwenye mchezo huo.

**JE, WAJUA?**



KIPIGO cha mabao 9-0 Liverpool ilichokitoa kwa Bournemouth juzi, kinaingia kwenye rekodi ya ushindi mkubwa kwenye Ligi Kuu England kikiungana na ushindi wa Manchester United 9-0 Southampton (Februari 2, 2021), Southampton 0-9 Leicester City (Oktoba 25, 2019), Manchester United 9-0 Ipswich Town (Machi 4, 1995).



# Taasisi za dini zaombwa kupambana na udumavu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amezitaka taasisi za kidini kushirikiana na serikali kupambana na tatizo la lishe na udumavu kwa kuwapa wananchi teknolojia bora za kilimo kulingana na hali ya hewa ya Dodoma.

Akizungumza aliposhiriki ibada ya Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Senyamule, alisema kumekuwa na fikra potofu kuwa Mkoa wa Dodoma una kame na baadhi wa watu kushindwa kujishughulisha na kilimo.

"Mkoa wa Dodoma hali ya udumavu ni asilimia 34 hii namba ni kubwa sana lazima tushirikiane kuhakikisha tunawawezesha wananchi teknolojia rahisi nakumbuka Nanenane mlionyesha umwagiliaji wa matone ya madumu elimu ile mkiipeleka vizuri kwa wananchi wataweza kulima mboga hatimaye kuondokana na udumavu," alisema.

Alisema endapo wananchi watapata elimu ya kilimo hicho itasaidia kupunguza tatizo la lishe kwa jamii na kutakuwa na chakula cha kutosha.

Aliwataka CCT kushirikiana na serikali kwa kuwa kuna mambo mengi ya kushirikiana katika kupeleka maendeleo kwa wananchi ili kuondoa umaskini miongoni mwa jamii.

"Mimi ninapoiangalia CCT siiangalii kama taasisi ya dini bali ni taasisi ambayo ina mchango mkubwa kwa jamii katika kupeleka maendeleo kwa jamii ya Watanzania na ninawafahamu mmefanya mambo makubwa katika kuisaidia serikali kutoa huduma kwa jamii," alisema.

Alisema serikali ina mpango wa kuanzisha kilimo cha umwagiliaji kwa Mkoa wa Dodoma na kwa Wilaya ya Chamwino kuna heka 8,000 na Bahi ni 2,700.

"Tunaanzisha kilimo cha pamoja (block farming) na kitaenda sambamba na ujenzi wa mabwawa makubwa na maghala ya kuhifadhia chakula."

"Dodoma tuna bahati kubwa sana kiwanda kikubwa cha mbolea kinajengwa na serikali imetoa ruzuku kwahiyo upatikanaji wa mbolea itakuwa rahisi sana kwa wananchi wa Dodoma," alisema.

Alihimiza taasisi hizo kushirikiana na serikali katika utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Hivi karibuni tutaanzisha kampeni maalumu ya utunzaji wa mazingira na upandaji miti tunaona serikali inafanya kazi kubwa katika ujenzi wa makao makuu ya nchi sisi jamii kazi yetu ni kutunza mazingira na upandaji miti," alisema.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu CCT, Mchungaji Moses Matonya, alisema wameona ni vyema wakaandaa ibada maalumu ya kumkaribisha Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na kumwelezea kazi kubwa wanayoifanya katika jamii.



Mkurugenzi wa Taasisi isiyo ya kiserikali ya Kaya Foundation, Annapili Ngome, akichangia mada katika semina ya kuongeza ushiriki wa wanawake, nafasi za maamuzi, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Semina hiyo iliandaliwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TBS yateketeza bidhaa zilizopita muda za mil. 100/-

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), Kanda ya Kati limeteketeza bidhaa za aina mbalimbali zikiwamo za vyakula na vipodozi vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 100 baada ya kukuta vikiuzwa huku vikiwa vimeisha muda wa matumizi.

Vipodozi vilivyoteketezwa ni vilivyopigwa marufuku kwenye soko la Tanzania kutokana na kuwa na viambata vya sumu ambavyo vina madhara ya kiafya kwa mtumiaji.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki mkoani Dodoma, Mkaguzi wa TBS, Domisiano Rutalala, alisema bidhaa hizo ziliteketezwa kwenye dampo la Chidaya na zilikamatwa katika halmashauri zote za mikoa ya Singida, Dodoma na Tabora, kipindi cha kuanzia Novemba, mwaka jana hadi Agosti, mwaka huu.

"Kwa bidhaa za vipodozi vyenye viambata sumu husababisha magonjwa muda mrefu, ikiwamo kuathiri ngozi, mfumo wa uzazi, ukuaji wa mtoto aliyeko tumboni na magonjwa ya saratani," alisema.

Alifafanua kuwa kaguzi ambazo zinafanywa na TBS ni endelevu katika mikoa yote ya Tanzania na kutoa wito wa wanunuzi kuhakiki bidhaa wanazonunua ili kujiridhisha kama zinakidhi matakwa ya matumizi kwa kuangalia muda wa mwisho wa matumizi na kuepuka kununua vipodozi vyenye viambata sumu.

Aliwataka wafanyabiashara wote wa vipodozi kutembelea tovuti ya TBS ambako watapata taarifa za vipodozi ambavyo havitakiwi kwenye soko la Tanzania.

"Hizi bidhaa tunazoteketeza unakuta walizinunua kwa gharama kubwa sana na kwa mujibu wa taratibu na sheria za TBS zipo faini ambazo wanatozwa kwa kukutwa na hizo bidhaa ambazo zimezuiwa kuuzwa kwenye soko," alisema.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara kuepuka tabia ya kuharibu tarehe ya mwisho ya matumizi au kubadilisha tarehe iliyowekwa ili kuepuka kupata hasara.

# Mama/babalishe wakumbushwa kupima afya

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Afya wa Jiji la Dodoma, Dk. Abdallah Mhia, amewataka mama na baba lishe kufuata sheria zinazotolewa na Halmashauri ya Jiji hilo ikiwamo kupima afya zao mara kwa mara na kuvaa sare wanapokuwa kazini.

Mhia aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye operesheni ya ukaguzi wa usafi katika masoko ya jiji hilo.

Alisema badala ya kusubiri kuburuzwa mahakamani na kutozwa faini, wahakikishe wanapima afya zao na kuvaa sare huku maeneo yao yakiwa safi ili kuepukana na magonjwa.

"Ninawaagiza kila siku mama na babalishe, wachoma chips na mishikaki na wauza nyama mabuchani kufuata maagizo wanayotakiwa kufanya kama vile kupima afya, usafi na kuvaa sare wanapokuwa kazini," alisema.

Naye Gwantwa Mbwile, Ofisa Afya Mazingira, Kata ya Viwandani jijini hapo, alisema elimu bado inahitajika kwa wajasiriamali ili kujisimamia wenyewe na kuepukana na faini wanazotozwa kwa mujibu wa sheria ndogo za jiji.

Alisema elimu hiyo ikitolewa mara kwa mara kwa upande wao watakuwa kwenye mazingira mazuri kiafya kwa kupima afya na kuvaa sare kwenye maeneo yao wanayofanyia kazi kuwa safi. "Sisi maofisa afya wa Jiji la Dodoma tunahakikisha tunatoa elimu kwa mama na babalishe kufuata sheria zote kama vile kuchemsha maji yao ya kunawa, kuvaa sare na kupima afya, kwa ajili ya kuwakwepesha wasilipe faini ya Sh. 50,000 hadi Sh. 300,000 au kuburuzwa mahakamani," alisema. Alisisitiza wafanyabiashara wa soko la Sabasaba wanafanya usafi kila siku badala ya kusubiri Jumamosi.

Alisema usafi huo uwe endelevu kwa kila mfanyabiashara ili kuweka mazingira yao safi badala ya kusubiri kusimamiwa na wakati mwingine kutozwa faini.





# Afariki dunia kwa moto akiwa amelala nyumbani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKAZI wa Soweto, Esther Lyanda (60), amefariki dunia akiwa amelala nyumbani kwake huku chanzo kikidaiwa kuwa ni moto.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Ruanda, Faraja Wila, alisema kuwa tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia juzi baada ya majirani kushtuka na kuukabili moto huo ambao hata hivyo walichelewa na kumkuta Esther akiwa ameshafariki.

Alisema Esther alikuwa anaishi peke yake kwenye nyumba hiyo na haikuwa rahisi kupata msaada wa haraka baada ya moto huo kuwaka hadi majirani waliposhtuka.

"Inavyoonyesha ni kwamba marehemu aliingia chumbani kwake kulala na aliweka moto kwenye kigae, sasa kuna uwezekano kwamba ndicho kilikuwa chanzo cha moto huo, moto umezimwa na kuokoa baadhi ya vitu, lakini imeshindikana kuokoa maisha ya mama huyu," alisema Faraja.

Ndugu wa marehemu walisema ndugu yao alikuwa anasumbuliwa na matatizo ya akili ambayo yalikuwa sio makubwa na wanaamini ajali hiyo ilitokea kwa bahati mbaya.

Mmoja wa ndugu hao, Bonface Moses shangazi wa marehemu, alisema mama huyo alikuwa anajitafutia kipato kwa kuokota chupa za plastiki na kuziuza na walikuwa wanaishi naye vizuri licha ya matatizo yake madogo ya akili.

Alisema asubuhi wakati anaenda kazini alipita katika eneo hilo na hakubaini chochote mpaka alipopigiwa simu akiwa kazini kwake kwamba shangazi yake ameungua.

"Sikuona moto na wala sikuona hata dalili ya moshi, nilipopigiwa simu nakuja nikakuta tayari majirani wamezima moto, lakini shangazi alikuwa tayari ameshafariki," alisema Bonface.

Baadhi ya majirani walisema walibaini kwamba kuna moto wakati sehemu kubwa ya vyombo vimeungua na bibi huyo tayari ameshafariki na kutoa taarifa kwa viongozi wa serikali kabla ya mwili kuchukuliwa na polisi.



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye ulemavu, Patrobas Katambi (kulia), akitoa maagizo kwa viongozi wa Kiwanda cha Saruji cha Mbeya (Mbeya Cement) mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya kushtukiza ambapo aliwataka kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi ili kuepuka madhara ya kiafya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kiwanda chapewa mwezi mmoja kuboresha mazingira

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye ulemavu, Patrobas Katambi, ametoa mwezi mmoja kwa uongozi wa Kiwanda cha Saruji cha Mbeya Cement kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi ili kupunguza madhara ya kiafya.

Katambi alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya kushtukiza kwenye kiwanda hicho kwa lengo la kukagua utekelezaji wa Sheria ya Afya na Usalama mahali pa kazi pamoja na mikataba ya kazi na utekelezaji wake.

Katambi aliongozana na maofisa mbalimbali wa serikali wakiwamo kutoka Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi (WCF), maofisa kutoka kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, maofisa wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA).

Akiwa kwenye kiwanda hicho, Katambi alibaini kuwa afya za baadhi ya wafanyakazi hasa wa kwenye uzalishaji ziko hatarini kutokana na kukosa vifaa vya uhakika vya kujikinga na vumbi linalotimka wakati wa uzalishaji.

Alisema hali hiyo ni hatari na inazalisha wagonjwa na wenye ulemavu na kuagiza maeneo hayo yarekebishwe ndani ya mwezi mmoja.

Aliagiza viongozi wa kiwanda hicho kutafuta mitambo ya kisasa zaidi ambayo wakati wa uzalishaji haizalishi vumbi jingi ili kupunguza zaidi madhara kwa wafanyakazi.

"Wakati mkiendelea kutafuta teknolojia za kisasa zaidi hebu jaribuni kuwalinda hawa wafanyakazi, wapatieni hata barakoa ili kupunguza madhara ya vumbi hili, mnatuzalishia walemavu na wagonjwa jambo ambalo sio kusudio letu," alisema Katambi.

Vilevile, aliutaka uongozi wa kiwanda hicho kutolipa kampuni zinazofanya nazo kazi kama hazitekelezi sheria za nchi na kushauri kwenye mikataba yao waweke kipengele kinachosisitiza utekelezaji wa sheria hizo.

Aliagiza maofisa wa OSHA kushirikiana na uongozi wa kiwanda hicho pamoja na vyama vya wafanyakazi wa kiwanda kuboresha mazingira ya utendaji kazi. Mwakilishi wa WCF, Mkoa wa Mbeya, Ayoub Bendera, alisema wamekuwa wakipata malalamiko mengi ya magonjwa kutoka kwa wafanyakazi wa kiwanda hicho kutokana na mazingira ya kazi.

Alisema wafanyakazi wanafanya kazi kwa muda mfupi na kuanza kuugua hali ambayo inaufanya mfuko huo kutumia fedha nyingi kuwalipa fidia.

"Tumekuwa tukipokea kesi nyingi sana za wafanyakazi kuugua wawapo kazini kwenye kiki kiwanda na tunalazimika kuwalipa fidia, kwahiyo tunaomba waboreshe mazingira ya kazi," alisema Bendera.

Kwa upande wake Kaimu Meneja wa OSHA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Uswege Faston, alisema mpaka sasa hawajatoa cheti cha usalama na afya mahali pa kazi kwa kiwanda hicho kutokana na kutotimiza baadhi ya masharti. Alisema kuna baadhi ya maeneo ni kiwanda chenyewe hakijatimiza masharti na kuna baadhi ni makosa ya kampuni ambazo kiwanda hicho kimeingia nayo mikataba.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda hicho, Khaled Ghareib, alisema wamekuwa wakijitahidi kufanya kazi kwa kuzingatia matakwa ya sheria za nchi, lakini kwa sehemu kubwa wanakwamishwa na kampuni wanazofanya nazo kazi.

Alisema watahakikisha wanatekeleza agizo la Naibu waziri ili kuendana na matakwa ya sheria za nchi pamoja na za kimataifa ili kuimarisha uzalishaji.

# Zaidi ya wanafunzi 900 washindwa kufanya 'Mock'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAFUNZI 951 wa Kidato cha Nne katika Mkoa wa Mbeya, hawakufanya Mtihani wa Utimilifu (Mock) ulioshirikisha mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo utoro na magonjwa. Ofisa Taaluma wa Mkoa wa Mbeya, Ally Masoud, alitoa taarifa hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha wadau wa elimu kilichokuwa na lengo la kufanya tathmini ya elimu katika mkoa huo na kutangaza matokeo ya mtihani wa utimilifu.

Kikao hicho kiliwashirikisha wakuu wa shule, waratibu elimu kata, maofisa elimu wa halmashauri, wakurugenzi wa halmashauri, maofisa kutoka Chama cha Walimu nchini (CWT) na maofisa kutoka Ofisi ya Mdhibiti Ubora wa shule Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Kati ya wanafunzi hao ambao hawakufanya mtihani huo uliofanyika mwezi Julai mwaka huu, wavulana walikuwa 504 na wasichana 447 na asilimia kubwa hawakufanya mtihani kwa sababu ya utoro.

Ambao hawakufanya mtihani huo kwa sababu ya utoro walikuwa 864, ugonjwa wanafunzi 50, vifo wawili na sababu nyingine 12, wasichana 23 hawakufanya mtihani kwa sababu ya kupata mimba.

Alisema wanafunzi waliokuwa wamesajiliwa kufanya mtihani huo walikuwa 26,726 na waliofanya walikuwa 25,775 ambao ni sawa na asilimia 96.44.

"Lengo letu ni kuhakikisha wanafunzi wote wanaokuwa wamesajiliwa kufanya mtihani wanafanya mtihani na wanafaulu vizuri, hawa wanafunzi ambao hawakufanya mtihani wana sababu mbalimbali na idadi inatofautiana kulingana na halmashauri," alisema Masoud.

Alisema lengo la mkoa huo ni kufikia ufaulu wa asilimia 100 kutoka 89 ya mwaka jana na kupandisha ufaulu kufikia wa GPA ya 3.4 kutoka GPA ya 3.6 ya mwaka uliopita.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Ernest Hinju, aliagiza wakuu wa shule kwa kushirikiana na wadau wengine zikiwamo bodi za shule kuhakikisha wanafunzi wote ambao hawakufanya mtihani kwa sababu ya utoro wanafuatiliwa ili warejee shuleni.

Aliwataka kuhakikisha wanahudhuria shuleni siku zote zilizobaki kabla ya kufanya mtihani wa taifa ili kuepuka kuwa miongoni mwa watakaosababisha ufaulu kuwa chini ikilinganishwa na malengo ya mkoa.

Kwa sasa zimebaki siku zaidi ya 80 ambazo wanafunzi hao watatakiwa kukaa darasani na kusoma na wenzao ili kuepuka kushindwa kufanya mtihani wa mwisho.

"Hawa wote ambao hawakufanya mtihani ndiyo wanaoweza kututengenezea daraja la sifuri na daraja la nne, sasa kwa siku zilizobakia kabla ya mtihani wa mwisho ni lazima tuwafuatilie na kuhakikisha wanahudhuria masomo," alisema Mwalimu Hinju.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka walimu kufundisha kwa kuzingatia miongozo na mitaala ili kuhakikisha lengo la serikali la kuzalisha wataalamu linafikiwa.

Homera aliwataka walimu kubadili mfumo wa adhabu kwa wanafunzi wanaofanya kazi kwa kuwapatia mitihani maalumu badala ya kuwapa adhabu ya viboko.

# Makamu wa Pili aahidi ushirikiano sekta binafsi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah, amesema, serikali ya Zanzibar itaendelea kushirikiana na taasisi binafsi kuwaletea wananchi maendeleo pamoja na kukuza uchumi wake.

Aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa kituo cha kukuza ujuzi kwenye sekta ya utalii (Zenj center of excellence for tourism- and hospitality), huko Michamvi Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema uwapo wa kituo hicho utasaidia kukuza sekta ya utalii kwa wananchi wa maeneo hayo na maeneo jirani watakao fika kujifunza.

Alisema ni ishara ya taasisi binafsi kuiunga mkono serikali kwenye sera ya uchumi wa buluu na sera hiyo inahitaji ushirikiano baina ya serikali kuu na sekta binafsi.

Hemed alisema kuwa taasisi hiyo itawasaidia wananchi wa Zanzibar kupata ajira za muda mrefu zitakazowasaidia kufanya shughuli zao kupitia sekta ya kitalii na kusaidia kukuza uchumi kwa kupitia wageni wanaoingia na kutoka nchini.

Aidha, serikali itaendelea kuwakaribisha wawekezaji kuekeza Zanzibar hasa katika sekta ya utalii kwa maslahi ya Wazanzibari.

Aliwataka wanafunzi wa kituo hicho kuutumia ujuzi na taaluma watakaopatiwa ili kuendana na soko la utalii duniani.

Makamu alisema Zanzibar ni nchi pekee ulimwenguni iliyobarikiwa kuwa na vivutio vingi vya kihistoria, hali ya hewa nzuri fukwe za kuvutia na kwamba ni vyema kuvitumia vitu hivyo ili kujiajiri na kuvitangaza kukuza soko.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhammed Mussa, alisema kuwa serikali tayari imeshatoa kibali kwa kituo hicho kuanzisha masomo na kinaendana na sera ya serikali kuwainua vijana kimaendeleo.

Waziri Lela aliwataka wamiliki wa kituo hicho kuhakikisha hatua zilizobaki ili kufanya mitihani ya mafunzo amali (VTA) na kuwataka kuanzisha vituo kama hivyo katika kisiwa cha Pemba kwa lengo la kuwakomboa vijana kutoka kwenye utegemezi na kujiajiri wanapomaliza masomo yao.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa kituo hicho, Toufiq Turki, alisema malengo makuu ya kituo hicho ni kuiunga mkono serikali kuu kwa kuwapatia mafunzo ya amali vijana hasa katika sekta ya utalii ili kujiajiri.

Alisema kuwa idadi ya wanafunzi 27 kutoka Unguja na Pemba imeshaanza kupatiwa mafunzo ya utalii na tayari hoteli mbalimbali nchini tayari zimeshajitokeza kutaka kuwaajiri vijana hao watakapomaliza mafunzo yao.



Wajumbe wa Sekretarieti ya Chama cha ACT-Wazalendo wakipitia majina ya wagombea wa ubunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA) Vuga visiwani Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ‘Marekebisho sheria zilizopitwa wakati muhimu’

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe, amesema kuna haja ya kufanyiwa marekebisho ya sheria mbalimbali zilizopitwa na wakati ikiwamo ya mtoto ya Zanzibar.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya kujadili Sheria ya Mtoto Zanzibar, kanuni na pensheni jamii kwa kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi iliyofanyika Baraza la Wawakilishi Chukwani nje kidogo ya mji wa Zanzibar.

Alisema kufanyiwa marekebisho kwa sheria hiyo ni muhimu hasa katika makosa ya udhalilishaji kwa watoto kupata mwarobaini.

Alisema Serikali ya Zanzibar inahimiza kila wizara kuzipitia sheria zake zote kwa ajili ya kuzirekebisha na kupata ufanisi zaidi.

“Tutoe michango ya kujenga sheria yetu ya mtoto na sheria zingine ikiwamo ya pensheni kwa sababu uzee haukwepeki nalo tuliwekee mustakabali mzuri kwa sababu waswahili wanasema uchonge mwiko ili usiungue mkono,” alisema.

Waziri Pembe alisema ni imani yake kwamba michango ya wajumbe hao itakuwa na manufaa makubwa katika sheria hiyo na pensheni ya wazee ili kuleta ufanisi.

Aliupongeza uongozi wa taasisi kuwalea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu (SOS) kwa ushirikiano wanaotoa kwa wizara hiyo hasa katika suala la mtoto.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Maryam Juma Sadalla, alisema lengo la mkutano huo ni kujadili Sheria ya Mtoto, kanuni pamoja na pensheni jamii ili kukusanya maoni na kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Aliiomba kamati hiyo kutoa maoni ya kuboresha pensheni jamii ambayo inagusa moja kwa moja watu muhimu ambao walikuwa na mchango mkubwa katika nchi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, Mohammed Ahmada Salum, alisema Sheria ya Mtoto namba 6 ya mwaka 2011 ni ya muda mrefu na ina mambo mengi, kwa sasa katika kumlinda mtoto kuna sheria zimekuja ambazo zina utofauti na sheria hiyo ya mtoto.

Alisema sheria ya ushahidi na sheria ya mahakama ya kadhi haiendani sambamba na sheria ya mtoto iliyopo hasa katika masuala ya malezi na ushahidi katika kesi za udhalilishaji kwa watoto.

Alisema bado hakuna muundo mzuri wa kuwafanya watoto kushirikishwa katika mashauri mengi yanayowahusu na upungufu uliopo ukifanyiwa kazi kutakua na sheria nzuri inayoenda sambamba na mahitaji ya watoto.

Mwanasheria Jabu Mbarouk Haji, kutoka Idara ya Ustawi wa Jamii, alisema Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2011 imeelezea mambo muhimu kwa mtoto ikiwa ni pamoja na maslahi bora, uamuzi wa maslahi ya mtoto, ushiriki wake na maoni yaliyotolewa, kutobaguliwa, haki ya kuwa na jina na utaifa, haki ya kuandikishwa kuzaliwa na haki zingine muhimu.

Akiwasilisha mada ya utekelezaji wa pensheni jamii, Mkuu wa Kitengo cha Pensheni Jamii, Aisha Abass Seif, alisema jumla ya wazee 21,263 Zanzibar wamelipwa pensheni kwa mara ya kwanza mpango ulipoanza mwaka 2016 na Unguja ni wazee 12,722 na Pemba 8,541.

# SMZ, SJMT zaja na mpango kudhibiti uvuvi bahari kuu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimeweka mpango wa udhibiti wa uvuvi wa bahari kuu na usimamizi wa mambo ya uvuvi hasa viumbe wa baharini ambao wapo ukingoni kutoweka.

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, alisema hayo mjini hapo, katika kikao cha kamati ya uongozi cha wizara hiyo baada ya uwasilishaji wa mpango pendekezwa wa usimamizi wa samaki jamii ya jodari.

Suleiman alisema mpango huu umekuja kwa lengo la kudhibiti ulaji wa kasa pamoja na kuondoa uvuvi holela wa viumbe wa baharini ambao wapo katika orodha maalumu ya usimamizi wa samaki aina ya papa, tuna na jodari kwa kupitia Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania (DSFA).

“Ikiwa watavuliwa samaki bila ya usimamizi maalumu ni viumbe ambao wanaweza kupotea na wasiwepo tena,” Suleiman alieleza.

Alisema kuwapo kwa mpango huo wa usimamizi kutasaidia mipango ya uwekezaji kwa ajili ya kuwekeza kwa kiasi gani na mwonekano wa baadaye katika kutekeleza miradi na sheria ya kimataifa ambazo tayari zimefunga mikataba na Indian Ocean Rim Association (IOR) na Tuna Commission.

Aidha, alisema serikali zote mbili zinaendelea kushajihisha katika kuwavutia wawekezaji ambao watavutiwa kuwekeza uvuvi wa bahari kuu kwa kufuata masharti, sheria na kanuni pamoja na miongozo ya kimataifa.

“Samaki aina ya jodari wana tabia ya kuhamahama na kupelekea kusafiri kwenda nchi nyingine baharini hivyo si jambo baya ambalo litatuwezesha uwekezaji katika kusimamia mpango huu na sheria,” alisema.

Ofisa Mkuu wa Uvuvi kutoka Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania, Ranwel Mbukwah alisema mpango huo utaleta faida kubwa kwa taifa kutokana na utaratibu uliowekwa wa usimamizi wa rasilimali ya uvuvi wa jodari na jamii zake akiwamo samsuri, papa na nduaro na kukiwa na usimamizi wa pamoja utaufanya uvuvi kuwa endelevu.

Kwa upande wao wadau wa kamati ya uongozi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, walisema mpango huo wanaendelea kuhusisha wataalamu mbalimbali wa wizara hio pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya Tanzania Bara kwa ajili ya kupokea maoni ili kupata kitendea kazi chenye mwongozo mzuri.

MAKALA MAALUM

# ‘Vijana Watanzania tafuteni majibu ya maswali magumu’

Na Mwandishi Maalum

KUNA wakati ili tuendelee tunahitaji ujasiri wa kusimama lakini si kwa kutoa majibu mepesi, bali majibu ya maswali magumu yakiwa majawabu huru. Tutoe majibu huru yasiyokuwa na harufu ya kupandikizwa.

Ni kwa bahati mbaya nchi yetu kitambo hatukujenga misingi ya ujasiriamali. Kwa mapinduzi makubwa yaliyotokea katika sekta ya mawasiliano, kwamba asilimia kubwa ya vijana wana vishikwambi mkononi, matarajio yangu halali vijana hawastahili kutumia mitandao ya kijamii kulalamika, bali waitumie kama fursa ya kujikwamua kiuchumi.

Kufikia hili, tunahitaji vijana kujitambua. Kila kukicha kijana atafute fursa. Ni vyema tuangalie tunapokwenda kabla ya kutoa majibu mepesi. Lazima tufikirishe akili kwanza! Kabla vijana hawajatafuta kusifiwa, waangalie misingi waliojijengea kwa nia ya kuwa na familia imara zitakazo kuwa na urithi wa kudumu. Vijana wabadili lugha na mijadala yao vijiweni. Mazungumzo yawe ni mipango ya maisha ya kwa sasa na siku zijazo.

Natoa hoja hii, kwa kuangalia mbali na kutanguliza maslahi mapana ya vijana wote wa Tanzania waliojiajiri kupitia sekta mbalimbali. Nawaheshimu na kuwapenda sana vijana, lakini kuna mahali tunakosea mno!

Hivi karibuni ndugu zetu Kenya walifanya uchaguzi. Kipindi chote cha kampeni, vijana hawakuwa wakiuliza maswali ya serikali itafutanyia nini, bali waliuliza serikali itajengaje fursa za wao kukua kiuchumi.

Ni bahati mbaya hapa kwetu kila siku kwenye mitandao ya kijamii na vijiweni, kila awaye ana gunia la lawama kwenda kwa serikali. Sioni tofauti kati ya vijana wa mwaka 1980 na sisi 2022. Ukifuatilia kushindwa huku kwa vijana kutafuta majibu ya masuala mazito yanayowakabili, jibu letu ni kuwa hatupo tayari kuwa rasmi, kujali kesho yetu.

Nasikitika, kwamba vijana wetu wako tayari kulipia gharama za kupofusha akili zao, sijui wanaita “connections”, tena kwa gharama kubwa badala ya kusaka masoko ya mchicha, mayai, utengenezaji wa tofali, ujenzi, uuzaji wa mazao mtandao au kutafuta uwakala na kazi nyingine nyingi zilizozagaa mtandaoni.

Inawezekana, narudia, inawezekana kuwa vijana wetu hawana utaalamu wa kutumia mtandao na hili linaweza kutumiwa kama sababu ya kutopata kazi za kufanya kupitia mtandaoni, lakini najiuliza nani aliwapa utaalam wa kutafuta “connections?” Walifundishwa na nani? Iweje wana utaalam huo, lakini hawana utaalam wa kutafuta kazi mtandaoni? Tuitumie vizuri mitandao itulinde.

Hii ni hatari mno, lakini imenifikirisha kuwa vijana wengi Watanzania hawaijui kesho yao na ujana hauwezi ukadumu na kukaa milele. Kuna msemo kuwa kazi inavyofanywa na nywele, ndicho chakula cha mvi siku za usoni. Vijana tusipoandaa mazingira yetu sasa, hakika tutakuwa na wakati mgumu milele.

Vijana inapaswa wajitambue. Tumesikia vijana madaktari tisa waliounganisha nguvu huko Kipunguni Dar es Salaam wakaanzisha zahanati. Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa, ameahidi kuwasaidia kutimiza ndoto yao. Yule anayewaza nje ya mstari wa kawaida ndiye anatoboa.



Vijana wakiperuzi katika mitandao. **PICHA: MTANDAO**

Narudia, kuna siku vijana wanakesha mtandaoni kutafuta connection ya dada yetu maarufu kwenye mitandao anayewajaza upepo bila mashiko. Hapa nikamkumbuka rafiki yangu Ruge Mutahaba, nikajisemea moyoni mwanangu pumzika salama na Semina za Fursa.

Kwanini tutafute majibu mepesi kwa ajili ya vijana wetu? Lipo tatizo mahali. Kwanza vijana tumekosa ushirikiano sisi kwa sisi hatupo pamoja. Vijana kukaa na kujisifu haisaidii.

Tumeshuhudia wengi wanapoteza muda katika kujaza akili upepo, ila maisha yanapobana wanaelekeza lawama Rais Samia Suluhu Hassan. Ni kweli serikali ina wajibu wa kuwaonyesha vijana fursa, ila kamwe haitafanya kazi kwa niaba ya mikono yako.

Tukiendelea hivi, itafika mahala ambapo naogopa kuwa kuna siku wanafunzi watafeli mitihani, pamoja na serikali kujenga shule, kuajiri walimu, kufuta ada na mengine mengi, vijana tusipojishughulisha tutamtupia lawama Rais Samia kwa kosa la wanafunzi kutoketi tukasoma wakaelewa waliyofundishwa darasani. Wengine watalalamika kuwa Rais hasomi masomo kwa niaba yao na wao wakashinda mitihani!

Sisi vijana hatuna budi ya kutambua tunao wajibu katika taifa. Vijana tunatakiwa kuleta mapinduzi ya fikra kwa kubadili mitazamo, fikra na dhana zinazoturudisha nyuma katika kujikomboa kiuchumi, ikiwamo utegemezi kwa Serikali, husda, kukatishana tamaa na kutoungana mkono.

Vijana tunatakiwa kukabiliana na changamoto za kiuchumi zilizo mbele yetu, ikiwamo ushindani mkubwa wa soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki, dunia ya utandawazi na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yajayo mbele yetu.

Sisi vijana hatuna budi kushikamana, kusaidiana na kuinuana kwa lengo la kuhakikisha tunaibua fursa mbalimbali za kiuchumi hapa nyumbani Tanzania.

Serikali ina wajibu kwetu sisi vijana kwa kuweka mazingira wezeshi ya kisera, kisheria na kitaasisi yanayochochea ustawi wetu, hifadhi ya jamii na kutuwezesha kufikia kilele cha ndoto zetu au ukomo wa uwezo, vipaji na vipawa vyetu katika nyanja zote. Hii iwe ni katika uongozi, biashara, uvumbuzi, ubunifu, sanaa na michezo, tunayo fursa hiyo.

Kama nilivyosema, serikali inatujengea vijana uwezo kwa kutupatia stadi muhimu za kiuongozi, biashara na kitaasisi tuweze kuendana na kasi ya mabadiliko ya dunia, kumudu ushindani katika Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki na kutuandaa kikamilifu kutoachwa nyuma na kukabiliana na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yajayo mbele yetu.

Serikali ya Awamu ya Sita imeongeze bidii kuhakikisha upatikanaji wa taarifa kuhusu fursa za elimu, uendelezaji vipaji, biashara na uchumi za nje zitokanazo na mkakati wa diplomasia ya uchumi ambapo inahakikisha zinatufikia. Kwa hapa Rais Samia hana mpinzani, bali kazi kwetu sisi vijana.

Serikali imeongeza kasi ya kuchochea upatikanaji wa mitaji kwa vijana, hususan biashara ndogo na kati kwa kuboreshe sera kwenye taasisi za fedha za umma na sekta binafsi kutukopesha sisi vijana kwa masharti nafuu. Tunasikia kinachoendelea katika sekta ya kilimo yalikojazwa mabilioni ya fedha zikisubiri sisi vijana tuchukue fursa hizi.

Kuna mipango ya kutunganisha na mifuko mbalimbali ya uwezeshaji iliyopo chini ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi la Taifa (NEEC), ambayo tunaikaribisha. Hapa nina wazo zito. Mama yangu mpendwa Rais Samia, ikikupendeza naomba uanzishe Benki ya Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Rais tunakuomba kufanya mapitio katika sera ya Ununuzi na Sheria ya Manunuzi ya Umma Mwaka 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2013 na kuelekeza walau asilimia 30 ya manunuzi ya bidhaa na huduma zifanywe na Vijana. Hapa utakuwa umetuongezea kasi wakati vijana tunazidi kusaka fursa. Mungu ibariki Tanzania.

***Asante sana.***
***Majibu mepesi kwenye majawabu huru.***
***Billal Saadat***
***0742 117302.***

HABARI KIMATAIFA

# Mlipuko homa ya nyanya waibuka India

**KERALA, INDIA**

WIZARA ya Afya ya India imethibitisha kuwa ugonjwa wa homa ya mafua ya nyanya ulioikumba nchi hiyo sio hatari kwa maisha na kwamba kwa sasa madaktari wanatibu dalili zake tu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na BBC, wizara hiyo ilitoa miongozo ya kuzuia, kupima na matibabu ya magonjwa kwa majimbo yote ndani ya nchi hiyo.

"Ikiwa mtu yeyote anashukiwa kuambukizwa, anawekwa karantini kwa siku tano hadi saba baada ya dalili na wazazi pia wanahimizwa kuwa waangalifu haswa kwa kufuatilia dalili za watoto wao," ilisema wizara hiyo.

Pia imeelezwa kuwa hadi sasa kuna kesi 100 za homa ya nyanya nchini India, ambapo 82 ni watoto chini ya umri wa miaka mitano, huku ikibainishwa kuwa eneo lililo na mlipuko mkubwa zaidi ni Kerala, ikifuatiwa na Tamil Nadu.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano wako katika hatari ya kuambukizwa kwasababu virusi vinaweza kuenea haraka kwa kugusana kwa karibu, kama vile kugusa sehemu chafu, kinyesi cha watu walioambukizwa na kula vitu vilivyo na virusi.

Iliongeza kuwa dalili zinazoonekana kwa watu walioambukizwa ugonjwa huo ni kutokwa na malengelenge makubwa mekundu ya mfanano wa nyanya na vipele na kwamba vikiguswa vinaleta maumivu, zingine ni uchovu, kichefuchefu, kutapika, kuhara, homa, maumivu ya viungo na mwili kuumwa.

Aidha, inaelezwa kuwa hivi sasa wanasayansi bado wanajaribu kujua sababu ya ugonjwa huo, huku nakala iliyochapishwa na jarida la The Lancet la Uingereza kuhusu masuala ya tiba, ikibainisha kwamba ugonjwa huo hauna uhusiano na virusi vya COVID-19.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kituo cha Tiba cha Hospitali ya Ramathibodi, iligundua maambukizo kwa mtoto wa mwaka mmoja na kaka yake mwenye miaka mitano kutoka Uingereza, ambao wazazi wao waliwapeleka watoto hao kutembelea ndugu India na kukaa kwa mwezi mmoja.

Taarifa ilieleza kuwa wiki moja baada ya watoto hao kurudi kutoka Kerala mwezi uliopita, wakabainika kuwa na homa hiyo, ambapo mmoja aliyetambulishwa kwa jina moja May alikuwa na vipele kwenye mikono na miguu yake, kama homa ya mafua ya nyanya.

Wazazi wa watoto hao waliviambia vyombo va habari kwamba, waliona vipele na watoto wakishikwa homa na kwamba wakiwa India walikuwa wakicheza na mtoto mmoja ambaye anadaiwa kuwa na ugonjwa huo.

Homa ya nyanya iligunduliwa kwa mara ya kwanza nchini India Mei 6, mwaka, ambapo Wizara ya Afya ya India ilithibitisha kisa cha kwanza katika wilaya ya Kollam.

**BBC**

# Mapigano makali yarindima Libya

**TRIPOLI, LIBYA**

RAIA mmoja ameuawa na wengine kadhaa kujeruhiwa katika mapigano makali kati ya makundi yenye silaha katika mji mkuu wa Libya Tripoli, ambayo yamekuwa yakiendelea katika mji huo na kuzua hofu ya vita.

Mapigano hayo yalizuka mwishoni mwa wiki iliyopita katika vitongoji kadhaa vya Tripoli magharibi, katikati ya mgogoro wa kisiasa unaochochewa na serikali mbili zinazopingana.

Taarifa iliyotolewa na serikali yenye makao yake makuu mjini Tripoli iliyahusisha mapigano hayo na kambi ya serikali pinzani, pamoja na kwamba mazungumzo yanahimizwa kufanyika ili kuepusha umwagaji damu katika miji mikuu.

Vyombo vya habari nchini Libya vilidai kuwa raia pia wameuawa, lakini hakuna idadi rasmi iliyotolewa.

Katika taarifa iliyochapisha na RFI jana, mapigano hayo yalisababisha uharibifu mkubwa katikati mwa mji mkuu, huku picha mbalimbali zikionyesha magari yaliyoteketea kwa moto na majengo ya makazi, misikiti na zahanati yakiwa yameharibiwa kwa risasi, vingine vikiwa vimeteketea kwa moto.

Serikali ya mjini Tripoli inayoongozwa na Abdelhamid Dbeibah, ilimshutumu mpinzani wake Waziri Mkuu Fathi Bachagha, ambaye yuko katikati mwa Sirte kwa kutekeleza vitisho vyake vya kuutwaa mji huo.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa tangu kuteuliwa kwake mwezi Februari na bunge lenye makao yake makuu Mashariki mwa nchi hiyo Bachagha amekuwa akijaribu bila mafanikio kuingia Tripoli ili kuanzisha mamlaka yake, huku akitishia kutumia nguvu kufanikisha hilo.

Bachagha anaungwa mkono na mbabe wa kivita Khalifa Haftar, mwanajeshi mwenye ushawishi mkubwa mashariki mwa Libya, ambaye vikosi vyake vilijaribu kuteka mji mkuu mwaka 2019.

Dbeibah, mkuu wa serikali ya mpito, alithibitisha kwamba atakabidhi madaraka kwa serikali iliyochaguliwa pekee.

Ujumbe wa Umoja wa Mataifa (UN) nchini Libya ulisema una wasiwasi mkubwa na mapigano katika vitongoji vinavyokaliwa na raia na kutaka uhasama huo kusitishwa mara moja.

Libya ilitumbukia katika machafuko baada ya maandamano na mapigano yaliyosababisha kuanguka kwa utawala wa Muammar Gaddafi mwaka 2011, pia nchi hiyo inatajwa kuwa haijawahi kuandaa uchaguzi wa urais.

***RFI***



Mwonekano wa majengo yaliyoharibiwa kutokana na machafuko yanayoendelea Libya. **PICHA: MTANDAO**

# Uchaguzi magavana Mombasa, Kakamega kufanyika leo

**MOMBASA, KENYA**

WAKAZI wa mjini Mombasa na Kakamega iliyoko Magharibi mwa nchini Kenya wanatarajia kupiga kura leo ya kuwachagua magavana baada ya kampeni za kujinadi kukamilika.

Uchaguzi wa ugavana wa Mombasa na Kakamega uliahirishwa Agosti 9, mwaka huu, siku ulipofanyika uchaguzi mkuu, kutokana na hitilafu zilizojitokeza kwenye karatasi za kupigia kura na kutangazwa siku nyingine Agosti 23 ambapo ilipofika tarehe husika suala hilo halikufanyika pia kutokana na changamoto mbalimbali.

Tume huru ya uchaguzi na mipaka (IEBC), kupitia mwenyekiti wake, Wafula Chebukati, ilisema ililazimika kuahirisha uchaguzi huo tena kutokana na madai ya vitisho na kunyanyaswa kwa maofisa wa tume hiyo.

Pia pamoja na kwamba wakazi wa Mombasa wanatarajia kufanya maamuzi ya kumchagua gavana wao mpya leo, juzi waliapishwa magavana wa kaunti zengine 45 huku zilisalia Kaunti ya Mombasa na Kakamega.

Wakati shughuli hizo zikiendelea wito wa amani ulitolewa kwa viongozi na raia kwa ujumla, huku wagombea wakitoa rai kwa wananchi kuwapigia kura katika maeneo mbalimbali ya Mombasa na Kakamega.

Maofisa wa IEBC walisema wanaendelea na mikakati ya kuhakikisha uchaguzi huo wa ugavana unafanyika kama ulivyopangwa, ambapo kinyang'anyiro kikali kinatarajiwa kati ya wagombea wa kiti hicho Hassan Omar Sarai wa Chama cha UDA ambaye aliwahi kuhudumu kama seneta wa Kaunti ya Mombasa na Abdul-Swamad Nassir wa Chama cha ODM aliyehudumu kama mbunge wa eneo bunge la Mvita.

***DW***

# RAIS SAMIA AIPONGEZA SIMBA QUEENS, TFF KUIPIGA TAFU CAF

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, akiipongeza Timu ya Soka ya Wanawake ya Simba, Simba Queens kwa kutwaa Ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) 'Samia Cup', Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao, ameahidi kukutana na viongozi wa klabu hiyo kwa ajili ya kuandaa mikakati ya kuelekea michuano Ligi ya Mabingwa Afrika ya Wanawake.

Simba Queens juzi ilitwaa ubingwa huo baada ya kuifunga She Corporate ya Uganda kwa bao 1-0 kwenye mechi ya Fainali ya CECAFA kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wanawake iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Katika salamu zake, Rais Samia amesema kuwa ubingwa huo umejenga heshima kwa soka la wanawake Tanzania na nchi kwa ujumla.

"Nawapongeza wanangu Simba Queens kwa ubingwa wa Afrika Mashariki (CECAFA 2022) kwa wanawake (Samia Cup). Mmejenga heshima kwa soka la Tanzania na nchi kwa ujumla. Nawatakia kheri katika Ligi ya Mabingwa Afrika 2022 itakayofanyika nchini Morocco," aliandika Rais Samia kwenye salamu hizo za pongezi kupitia mtandao wa twitter.

Rais Samia ndiye mdhamini wa michuano hiyo ambayo kwa sasa inajulikana kama 'Samia Cup', ambapo ametoa zawadi za pesa kiasi cha dola za Kimarekani 60,000 kwa washindi watatu, bingwa akitwaa dola 30,000, mshindi wa pili dola 20,000 na wa tatu dola 10,000.

Bao pekee kwenye mechi hiyo, lilifungwa kwa mkwaju wa penalti na kiungo mkabaji raia wa Kenya, Vivian Corazone, baada ya Mrundi Asha Djaffar kubwagwa ndani ya eneo la hatari na beki mmoja wa She Corporate.

Kwa ubingwa huo, Simba Queens inakwenda kuuwakilisha Ukanda wa CECAFA kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika nchini Morocco Oktoba mwaka huu ambayo itakuwa na timu nane ikatayochezwa kwa makundi mawili kwa kugawanywa timu nne kila kundi.

Simba Queens ilianza michuano hiyo kwa kuifunga GRFC ya Djibouti mabao 6-0, ikaichapa She Corporate ambayo ilikuwa nayo pamoja kwenye Kundi B mabao 2-0, kabla ya kuichapa Yei Joint ya Sudan Kusini mabao 4-0 na kutinga nusu fainali ikiwa inaongoza kundi.

Kwenye mechi ya nusu fainali iliichakaza AS Kigali mabao 5-1, kabla ya kushinda bao 1-0 kwenye mechi ya fainali.

Kwa upande wa Katibu Mkuu wa TFF, Kidao, akizungumza na gazeti hili jana, mbali na kuwapongeza wachezaji, benchi la ufundi na viongozi wa Simba kwa kuiheshimisha nchi kutokana na kutwaa ubingwa huo, alisema wakutana na viongozi wa klabu hiyo kwa ajili ya kuona wanavyojipanga na utayari wao kwenye michuano hiyo.

"Tunawapongeza Simba Queens kwa kupambana na kuhakikisha Kombe la CECAFA linatua ndani ya ardhi ya Tanzania, lakini sasa ni wajibu wetu kukutana na viongozi wa Simba kwa ajili ya kuona jinsi gani timu hiyo inaenda Morocco kupambania Ukanda huu wa CECAFA katika Ligi ya Mabingwa Afrika ya Wanawake," alisema Kidao.

Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, pia alilipongeza benchi la ufundi na wachezaji kwa kufanikiwa kutimiza malengo yao ya kutwaa taji hilo kwa mara ya kwanza.

"Hatutaishia hapa, Simba malengo yetu ni kufanya vizuri katika michuano ya kimataifa na sasa jicho letu linahamia nchini Morocco kuhakikisha tunafanya usajili kulingana na mahitaji ya kocha Sebastian (Nkoma)," alisema.

# Travel Link kusafirisha mashabiki kwenda Kombe la Dunia Qatar

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Travel Link Tanzania Limited, imeandaa kifurushi cha bei nafuu kwa ajili ya usafiri na malazi kutoka Dar es Salaam kwenda Doha nchini Qatar kushuhudia Kombe la Dunia kuanzia Novemba mwaka huu.

Akizungumza mjini Dar es Salaam jana, Meneja Mauzo na Masoko wa Kampuni ya Travel Link, Fatema Lalji, alisema Watanzania wanaotaka kwenda Qatar watalipa kati ya dola 2,000 (sawa na Sh. milioni 4.6) na dola 5,000 (Sh. milioni 11.2) kwa ajili ya tiketi ya ndege kwenda na kurudi, usafiri mpaka viwanja vya ndege na gharama za hoteli.

Lalji alisema wasafiri hao watatumia ndege za makampuni ya Qatar Air, Emirates, Oman Air na Fly Dubai na kwamba mashabiki hao wa soka watanunua tiketi za kuingia viwanjani kupitia tovuti ya Shirikisho la Soka Duniani (FIFA). "Mara hii kifurushi chetu hakitajumuisha tiketi za kuingia viwanjani kwani FIFA wanaziuza wenyewe kwa njia ya mtandao, kwa hiyo kila mmoja atanunua moja kwa moja toka kwao," alisema Lalji.

Meneja huyo wa Mauzo na Masoko wa Travel Link, aliongeza kwamba wasafiri watakaopanda ndege za Qatar Air watasafiri moja kwa moja kwenda Qatar wakati wale wa Emirates, Fly Dubai na Oman Air watapitia Dubai na Muscat.

"Tunawasihi Watanzania wanaotaka kwenda kuangalia mechi za Kombe la Dunia Qatar kufanya booking sasa ili kuepuka gharama na usumbufu siku zikikaribia Novemba," Alishauri huku akiwaomba Watanzania kuwasiliana na Travel Link moja kwa moja kupitia ofisi zao Dar es Salaam katikati ya jiji, Kariakoo, Arusha, Dodoma na Mwanza.

"Lakini wateja wanaweza kuwasiliana nasi kwa njia ya mtandao kupitia tovuti yetu ya www.travellink.co.tz," alisisitiza meneja huyo wa Travel Link.

Kampuni ya Travel Link ilianzishwa mwaka 2005 na mfanyabiashara, Imtiaz Lalji ambaye ni mwenyekiti na mkurugenzi mtendaji. Kampuni hiyo ambayo makao makuu yake yapo Dar es Salaam ni mwanachama wa shirika la usafirishaji kwa njia ya anga duniani (IATA), Tanzania Society of Travel Agents (TASOTA) na Wildlife Conservation Society of Tanzania (WCST).




Meneja Mauzo na Masoko wa Travel Link Tanzania Limited, Fatema Lalji, akizungumza Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Jang'ombe yatambulisha 28 ikitoka sare

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Taifa Jang'ombe inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar imeutumia mchezo wake wa kirafiki dhidi ya Azam FC kutambulisha kikosi chake cha wachezaji 28, kwa ajili ya msimu mpya wa 2022/23 utakaoanza Septemba 5, mwaka huu.

Katika mchezo huo wa kirafiki uliochezwa katika Uwanja wa Amaan, timu hizo zilitoka sare ya bila kufungana.

Taifa Jang'ombe ilitambulisha kikosi chake cha msimu mpya ambacho ndani yake kulikuwa na wachezaji 15 ambao ndio wapya waliowasajili msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa timu hiyo, Haji Kiduka, alisema kupitia mchezo wao huo dhidi ya Azam FC wanaamini timu yao itafanya vizuri katika Ligi Kuu Zanzibar inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

"Kikosi chetu kinajumla ya wachezaji 28 na ni matumaini yetu wachezaji hawa kwa muda waliojiandaa wataenda kufanya vizuri katika michezo yetu ya ligi huku wakijua lengo letu ni kupata ubingwa," alisema.

# Twaha Kiduku kuzipiga na bondia wa Misri

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Twaha Khassimu maarufu Twaha Kiduku, anatarajia kutetea mkanda wake wa Ubingwa wa UBO Afrika dhidi ya Abdo Khaled wa Misri.

Pambano hilo linatarajiwa kufanyika Septemba 24, mwaka huu na kupewa jina la 'Mtwara Ubabe Ubabe 2', litafanyika mkoani Mtwara kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona.

Khaled ni bondia namba moja nchini Misri katika uzito wa Super Middle, mwenye rekodi ya kucheza jumla ya mapambano 12 akishinda saba kati ya hayo sita kwa KO, akiwa amepoteza mapambano manne tu mawili ni kwa KO, na ametoka sare mara moja.

Mara ya mwisho Kiduku kupanda ulingoni ilikuwa ni Machi mwaka huu baada ya kumtwanga kwa pointi, Alex Kabangu wa DR Congo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BELLINGHAM ATAKIWA LIVERPOOL
LIVERPOOL imeingia makubaliano ya mdomo na kiungo wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham ili ajiunge pale Anfield katika dirisha la Januari. ***(Football Insider)***

### AJAX YAKOMAA KWA ANTONY
KLABU ya Ajax inataka Manchester United itoe kitita cha pauni milioni 84.8 kwa ajili ya winga wa Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 22. ***(Mail)***

### REGUILON HUYOOO ATLETICO
MLINZI wa Tottenham Hotspur, Sergio Reguilon mwenye umri wa miaka 25, anakaribia kutua kwa mkopo Atletico Madrid, kuziba pengo la beki wa kushoto, mwenye umri wa miaka 24, Renan Lodi, aliyejiunga Nottingham Forest. ***(Times)***

### DUBRAVKA ANAITAKA UNITED
GOLIKIPA wa Slovakia, Martin Dubravka mwenye umri wa miaka 33, ameiambia Newcastle United kwamba, anataka kuondoka na kujiunga na Manchester United. ***(Sky Sports)***

### NEVES AFUATILIWA LIVER
LIVERPOOL inamfuatilia kiungo wa Wolves na Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 25, pamoja na kiungo wa RB Leipzig na Austria, Konrad Laimer mwenye umri wa miaka 25. ***(90min)***

### BARKLEY HATAKIWI CHELSEA
CHELSEA inafikiria kuvunja mkataba wa kiungo wa England, Ross Barkley pale Stamford Bridge, ambapo kwa sasa nyota huyo analipwa mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki. ***(Sun)***

### JANUZAJ KUREJEA EPL
KLABU ya West Ham inazungumza na winga wa zamani wa Manchester United, Adnan Januzaj ili kumrejesha Ligi Kuu England, ambapo Mbelgiji huyo mwenye miaka 27 yuko huru kuondoka Real Sociedad. ***(Talksport)***

### BUONANOTTE NA BRIGHTON
KLABU ya Brighton inamtaka kinda wa Rosario Central na Argentina, Facundo Buonanotte mwenye umri wa miaka 17 na wako tayari kutoa pauni milioni 3. ***(Athletic)***

### GNONTO AWINDWA LEEDS
KLABU ya Bournemouth inataka kuizidi kete Leeds United katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Zurich, Willy Gnonto mwenye umri wa miaka 18. ***(Football Insider)***

### LOKONGA AMULIKWA ROMA
KIUNGO wa kati wa Arsenal, Albert Sambi Lokonga, mwenye umri wa miaka 22, yuko kwenye orodha ya wachezaji wanaowaniwa na Jose Mourinho katika klabu ya AS Roma. ***(AS Roma Live, via Express)***

### ADAMS AWEKEWA NGUMU
KOCHA wa Southampton, Ralph Hasenhuttl amesema mshambuliaji, Che Adams mwenye umri wa miaka 26, hauzwi msimu huu. ***(Daily Echo)***

### PALMER KUNG'OLEWA CITY
KIUNGO wa kati wa Manchester City na England, Cole Palmer mwenye umri wa miaka 20, anasakwa kwa mkopo wa msimu mzima na Borussia Dortmund. ***(Sun)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: NI KAWAIDA KWA HAALAND KUFUNGA HAT-TRICK

Alikuja kwa ajili hiyo, kile ambacho amefanya, amekifanya maisha yake yote akiwa...

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amebainisha sifa za 'ajabu' za Erling Haaland baada ya hat-trick yake kuiwezesha Manchester City kuibuka na ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya Crystal Palace, Jumamosi.

Man City walikuwa wamefungwa 2-0 hadi mapumziko katika kile kilichotishia kurudiwa kwa ziara ya Palace kwenye Uwanja wa Etihad kama msimu uliopita.

Hata hivyo, Bernardo Silva alipunguza idadi ya mabao muda mfupi baada ya kuanza kipindi cha pili na Halaand akafunga mabao matatu na kufanya mabadiliko makubwa kwenye mchezo huo.

Ingawa Guardiola alisema rekodi ya mabao ya Haaland haijawahi kutiliwa shaka, alisisitiza kwamba, alifurahishwa zaidi na lugha ya mwili ya mshambuliaji huyo baada ya timu yake kufungwa 2-0.

"Alikuja kwa ajili hiyo (kufunga mabao muhimu), kile ambacho amefanya maisha yake yote," alisema kocha huyo raia wa Hispania.

"Namba za mtu huyu zinakuwa wazi. Jambo la muhimu zaidi ni kuwa ametulia kikamilifu, mtu mnyenyekevu sana. Anazungumza zaidi na wachezaji wenzake.

"Ninachopenda kwa Erling ni kwamba bado tunafahamiana. Bado tunahitaji muda zaidi. Niliona lugha yake ya mwili tukiwa nyuma kwa mabao 0-2 alivyokuwa akiwatia moyo wenzake.

Mabao matatu ya raia huyo wa Norway ndio ilikuwa hat-trick yake ya kwanza katika jezi za City, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, alifichua fahari yake katika mafanikio hayo baada ya ushindi huo.

"Ilikuwa wakati wa kujivunia kwangu na familia yangu," alisema Haaland,

"Furaha... hisia ya kushangaza kufunga mabao matatu, hat-trick."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI

VALENCIA
VERSUS
ATLETICO MADRID

1 | 3.89
X | 3.23
2 | 1.99

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP: KUIFUNGA MABAO 9 BOURNEMOUTH SI DHARAU



**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesisitiza kuwa hakuwahi kuidharau Bournemouth baada ya timu yake kufikia rekodi ya ushindi wa Ligi Kuu ya England kwa kushinda 9-0, Jumamosi.

'Wekundu' hao walikuwa na wafungaji nane tofauti huku timu ya Klopp ikipata ushindi wa kwanza katika msimu wa Ligi Kuu England baada ya kuanza kampeni kwa kusuasua.

Vijana Stefan Bajcetic na Bobby Clark pia walicheza mechi yao ya kwanza kwa jezi za Liverpool huku timu hiyo ya Anfield ikiibuka na ushindi huo mnono.

Klopp baada ya mchezo huo asisitiza kwamba kila mara ilikuwa ni juu ya timu yake kufanya vizuri na haikuwa kudharau dhidi ya timu hiyo ya kocha, Scott Parker.

"Tulitaka kuonyesha hisia. Tuwe wenyewe," alisema Mjerumani huyo.

"Kuwa toleo bora la sisi wenyewe. Tunacheza kwa njia maalum. Tulifunga mabao mazuri. Mchezo ulitulia na tukaendelea kufunga. Ilikuwa ni kuendelea.

"Si kuidhalilisha Bournemouth. Ni juu ya kuweka mpinzani chini ya shinikizo. Ningeweza kuleta watoto, wanastahili sana. Harvey (Elliott) ni mchezaji maalum. Kila kitu kilikuwa sawa sana."

# Arteta asifu mashabiki wa Arsenal

**LONDON, England**


MIKEL Arteta amesifu jukumu ambalo mashabiki wa Arsenal walionyesha katika ushindi wao dhidi ya Fulham pale kwenye dimba la Emirates, Jumamosi.

Mabao ya Martin Odegaard na Gabriel yakiwavuta kupita kwenye shimo walilochimbiwa na Alexandar Mitrovic kipindi cha pili.

'Washikabundi' hao walitoka nyuma na kushinda mchezo huo ambao Arteta anaamini wachezaji wake walitumia akili na nguvu baada ya makosa ya Gabriel.

Mbrazil huyo alinaswa kwenye ukingo wa eneo la hatari na Mitrovic, ambaye alimnyang'anya mpira na kufunga bao la kwanza - na Arteta alisisitiza beki huyo hapaswi kulaumiwa.

Akizungumza na waandishi wa



habari baada ya mchezo huo, alisema: "Nimefurahishwa sana na uchezaji, mtazamo, na mawazo ambayo timu ilionyesha. Tulikuwa juu ya mchezo, ilikuwa juu ya uvumilivu na sababu tulistahili, lakini tulikuwa na shida na makosa.

"Tulifanya makosa, ilitugharimu, lakini timu ilionyesha kwamba inapambana na Gabby alisawazisha makosa na tulipata msaada wa ajabu kutoka kwa mashabiki uwanjani."

"Mwitikio wa kila mtu na hasa baada ya kuwa nyuma, mwitikio wa uwanja, hutoa msaada kwa mchezaji, imani, halafu mchezaji anapaswa kuonyesha ujasiri wa kuendelea kucheza.

"Ni juu ya jinsi ya kucheza na nimefurahishwa sana. Jinsi alivyo (Gabriel) alibadilika kiakili, jinsi anavyokaribia kila siku, ni tofauti na mwaka mmoja au miwili iliyopita.

"Anajiangalia kila siku. Soka ni kitu muhimu zaidi katika maisha yake mbali na binti yake na familia yake. Jinsi anavyobadilika kila siku katika tabia zake na ni kiasi gani anataka kuwa mmoja wa wachezaji bora."

Matokeo hayo yameifanya Arsenal kurejea kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England.

Y | CHEZA USHINDE KASINO

# NBC, AMREF WAANDAA MARATHON KUUNGA MKONO 'UZAZI NI MAISHA'

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) kwa kushirikiana na Shirika la Amref Health Africa Tanzania, na Wizara ya Afya ya Zanzibar, wameendesha Kampeni ya 'Uzazi ni Maisha Wogging Marathon' katika Uwanja wa Sheikh Amani, Zanzibar, Tanzania.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alikuwa mgeni rasmi wa tukio hilo la Matembezi, Mbio Fupi na Ndefu (Wogging (Walk-Jog-Run)).

Kwa kauli mbiu: "Changia Vifaa Tiba kwa Uzazi Salama" matembezi, mbio fupi na ndefu (kwa kifupi 'wogging') zilizopata umaarufu zilikazia kutoa elimu kuhusu upungufu uliopo katika sekta ya afya na kukusanya fedha ili kusaidia jitihada za serikali katika kuhakikisha kwamba vifaa tiba na dawa kwa uzazi salama vinapatikana katika vituo vya afya vilivyobainishwa hapa Zanzibar.

Tukio hilo lililolenga kuhamasisha taasisi za umma, kampuni na sekta binafsi, watu binafsi pamoja na wadau wengine kuchangia na kutoa msaada wa vifaa tiba na dawa kwa uzazi salama visiwani hapo, liliwawaleta pamoja zaidi ya washiriki 4,000 wakiwamo maofisa wa ngazi za juu wa kampuni, wanadiplomasia, washirika wa maendeleo, maofisa wa serikali, vyombo vya habari na watu binafsi ambao waliotoa ahadi na kueleza utayari wao wa kusaidia kuchangia kampeni hii kupitia njia mbalimbali za utoaji msaada.

Katika kipindi cha miaka mitatu, Kampeni ya Uzazi ni Maisha Wogging, inalenga kukusanya zaidi ya shilingi bilioni moja ikiwamo misaada ya vitu, fedha taslimu na ahadi za kutoa misaada ya vifaa tiba kwa uzazi salama. Kampeni itaendeshwa kwa miaka mitatu huku kukiwa na ushiriki wa wadau mbalimbali hadi hapo lengo litakapofikiwa.

Mgeni rasmi wa tukio hilo, Dk. Mwinyi, alipongeza juhudi za Amref kwa kubuni njia hiyo ya kipekee na kuwaasa wadau zaidi kushiriki ili kuhakikisha wanakuwa sehemu ya upatikanaji wa vifaa tiba na dawa kwa ajili ya uzazi salama hapa Zanzibar.

"Idadi ya vifo vinavyotokana na matatizo ya uzazi vinavyowaathiri moja kwa moja kinamama na watoto wachanga bado iko juu hapa Zanzibar, ikiwa ni vifo vya kinamama 267 kati ya vizazi hai 100,000 kwa mwaka; na wastani wa vifo 28 vya watoto kati ya vizazi hai 1,000 kwa watoto wachanga (kutokana na takwimu za HMIS 2017)," alisema.

"Nimetaarifiwa, kupitia kampeni hii ya Uzazi ni Maisha, jumla ya vituo vya afya 28 vitapata vifaa tiba ambayo ni sawa na asilimia 40.5% ya vituo vyote vinavyotoa huduma ya mama na mtoto katika vijiji vilivyo hapa Zanzibar. Namhimiza kila mmoja ajitahidi kuwa sehemu ya mpango huu mwema na kuleta mafanikio kwa serikali yetu ya Zanzibar."



Mgeni rasmi Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi (kushoto), akimkabidhi cheti cha pongezi Mkurungezi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, jana. Benki hiyo ni mdhamini mkuu wa matembezi ya 'Uzazi ni Maisha Wogging Marathon' kwa kushirikiana na Shirika la Amref Health Africa Tanzania na Wizara ya Afya ya Zanzibar, zilizofanyika katika Uwanja wa Sheikh Amani, Zanzibar. **MPIGAPICHA WETU**

# Mkazi wa Geita alamba milioni 5.4/ Sportpesa

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Geita, Enos Paul Nzagamba, amekuwa Mtanzania wa kwanza kushinda mara nne Jackpot Bonus za Sportpesa, safari hii akiondoka na kitita cha Sh. 5,441,202.

Akizungumza wakati wa makabidhiano ya hundi katika ofisi za Sportpesa, Oysterbay jijini Dar es Salaam, Nzagamba alisema alianza kucheza mwaka 2020 na mpaka sasa ni mara yake ya nne kushinda vitita vya Jackpot Bonasi.

''Mimi ni mmoja wa wapambanaji ambaye kwa miaka hii miwili nimekuwa napambania kushinda Jackpot kubwa kiasi kikubwa kikiwa zaidi ya milioni 10, lakini mara zote naishia kwenye Jackpot Bonasi ambazo kwa kiasi kikubwa zinanibusti na kuendelea kupambana,'' alisema.

Anaendelea kusema kwa takriban miezi mitatu alikuwa amesimama kucheza baada ya Jackpot kubwa ya bilioni moja na ushee kuliwa.

''Unajua nilipambana sana wakati Jackpot ile kubwa ikiwa hai. Nashukuru hata sasa mmetuwekea Supa Jackpot ya mechi 17 ambayo imeanzia bilioni moja, hivyo imenipa ari ya kuipambania tena.

''Kwanza niwapongeze Sportpesa kwa ubunifu wenu katika michezo hii ya kubashiri. Mmekuwa na ubora ambao wengine itawachukua muda mrefu. Hii Jackpot mpya ya Supa Jackpot imepanua wigo mpana wa wachezaji kama sisi kupata fursa ya kuchagua ni kiwango gani tupambanie,''alisema Nzagamba.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 29/08/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1509 | FC Metalist Kharkiv vs FC Ingulets | 2.36 | 3.14 | 2.79 |
| 13:00 | 3547 | Jeonbuk Hyundai vs Pohang Steelers | 2.44 | 3.19 | 2.65 |
| 17:00 | 1698 | Altrincham vs Chesterfield | 3.29 | 3.34 | 2.07 |
| 17:00 | 2078 | Dorking Wanderers vs Boreham Wood | 2.50 | 3.50 | 2.50 |
| 17:00 | 2143 | Aldershot vs Maidstone | 2.79 | 3.39 | 2.32 |
| 17:00 | 2785 | York City vs Oldham | 2.82 | 3.47 | 2.26 |
| 17:00 | 2962 | Wealdstone vs Yeovil | 2.47 | 3.18 | 2.74 |
| 17:00 | 3431 | FK Liepaja vs Rigas Futbola Skola | 3.00 | 3.34 | 2.14 |
| 17:00 | 4096 | Southend vs Maidenhead U | 1.75 | 3.57 | 4.26 |
| 17:00 | 4468 | Notts County vs Solihull Moors | 2.24 | 3.43 | 2.88 |
| 17:00 | 4567 | Torquay vs Woking | 2.23 | 3.32 | 2.98 |
| 17:00 | 5113 | Scunthorpe vs Halifax | 2.53 | 3.23 | 2.63 |
| 17:00 | 5962 | Dagenham and Redbridge vs Bromley | 2.09 | 3.38 | 3.23 |
| 18:00 | 4591 | CSC Dumbravita vs CSA Steaua Bucuresti | 3.68 | 3.53 | 1.83 |
| 19:00 | 2031 | Akritas Chlorakas vs Omonia Nicosia | 4.95 | 3.79 | 1.66 |
| 19:00 | 3330 | Mjondalen vs Sandnes Ulf | 2.46 | 3.39 | 2.51 |
| 19:00 | 3387 | IK Start vs Grorud IL | 1.23 | 5.69 | 9.22 |
| 19:00 | 3713 | Asteras Tripolis vs Olympiakos | 4.51 | 3.31 | 1.81 |
| 19:00 | 4047 | Bryne vs Raufoss | 2.30 | 3.48 | 2.65 |
| 19:00 | 4778 | Skeid Fotball vs Kfum Oslo | 3.33 | 3.58 | 1.92 |
| 19:00 | 5526 | Brann vs Ranheim | 1.13 | 7.10 | 12.83 |
| 19:15 | 4809 | Konyaspor vs Fenerbahce | 3.28 | 3.48 | 2.07 |
| 19:15 | 5455 | Barnet vs Eastleigh | 1.94 | 3.54 | 3.49 |
| 19:20 | 2945 | Qatar SC vs Al-Shamal | 2.76 | 3.25 | 2.33 |
| 20:00 | 1820 | Brondby vs Midtjylland | 3.27 | 3.37 | 2.12 |
| 20:00 | 2539 | Arsenal Tula vs Yenisey Kr | 1.90 | 3.39 | 3.58 |
| 20:00 | 2681 | Mafra vs Sporting Farense | 2.54 | 3.14 | 2.69 |
| 20:00 | 3458 | Duisburg vs VfB Oldenburg | 1.99 | 3.44 | 3.49 |
| 20:00 | 5210 | Coca Cola vs Misr Lel Makasa | 1.25 | 5.44 | 11.08 |
| 20:00 | 5344 | AEK Larnaca vs Doxa Katokopia | 1.46 | 4.33 | 6.45 |
| 20:10 | 1749 | Djurgardens IF vs Elfsborg | 1.69 | 3.87 | 4.02 |
| 20:15 | 2554 | Hapoel Hadera vs Maccabi Tel Aviv | 6.47 | 4.22 | 1.41 |
| 21:00 | 1270 | Universitatea Craiova vs Botosani | 1.86 | 3.36 | 4.11 |
| 21:00 | 1459 | Aegir vs Haukar | 1.73 | 4.23 | 3.49 |
| 21:00 | 3231 | Heracles Almelo vs Maastricht | 1.22 | 6.18 | 9.96 |
| 21:00 | 4081 | Sacachispas FC vs Almirante Brown | 3.29 | 2.90 | 2.21 |
| 21:00 | 4929 | Vitoria Guimaraes vs Casa Pia Atletico | 1.99 | 3.26 | 3.77 |
| 21:00 | 5002 | Granada vs Villarreal B | 1.63 | 3.66 | 5.22 |
| 21:00 | 5616 | Cadiz CF vs Athletic Bilbao | 3.64 | 3.03 | 2.15 |
| 21:00 | 5784 | Jong Utrecht vs Willem II Tilburg | 4.99 | 3.99 | 1.58 |
| 21:45 | 3019 | Sligo Rovers vs Dundalk FC | 2.81 | 3.20 | 2.32 |
| 21:45 | 3188 | Bohemians FC vs St Patricks | 2.39 | 3.15 | 2.75 |
| 21:45 | 4891 | Shelbourne vs Derry City | 3.39 | 3.14 | 2.05 |
| 21:45 | 4951 | Como vs Brescia | 2.80 | 3.20 | 2.44 |
| 21:45 | 5026 | Besiktas vs Sivasspor | 1.52 | 4.22 | 5.62 |
| 22:00 | 2142 | Sedan vs Red Star | 3.33 | 3.13 | 2.15 |
| 22:15 | 2436 | Valur vs Fram Reykjavik | 1.45 | 4.51 | 5.29 |
| 23:00 | 2645 | Las Palmas UD vs FC Andorra | 1.69 | 3.56 | 4.81 |
| 23:00 | 2779 | Valencia vs Atletico Madrid | 3.89 | 3.23 | 1.99 |
| 23:15 | 2426 | FC Vizela vs Gil Vicente | 2.44 | 3.22 | 2.82 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Agosti 29, 2022
Nipashe



**Guardiola: Ni kawaida kwa Haaland kufunga hat-trick**

TUMELIBEBA...




Nahodha wa Simba Queens, Fatuma Issa 'Fetty Densa', akiwa amenyanyua kombe juu na kusherehekea na wachezaji wenzake baada ya kutwaa ubingwa wa kuwania kufuzu Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), kwa kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya She Corporate Uganda kwenye mchezo wa fainali uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SONG ATABIRI MAKUBWA KWA WACHEZAJI SIMBA

●●●Akunwa na vipaji, awapa mbinu za kucheza Ulaya, asema kama wakikaza buti...

**Na Saada Akida**

KIUNGO mkabaji wa Klabu ya AS Arta/Solar 7 ya Djibouti, Mcameroon Alex Song, amesema kikosi cha Simba kinaundwa na wachezaji wengi wenye vipaji na kwamba kama watakuwa wanajituma zaidi muda utaongea kabla ya kupata nafasi ya kucheza soka la kulipwa katika klabu kubwa za nje.

Song aliyewahi kuzichezea klabu mbalimbali barani Ulaya zikiwamo Arsenal na Barcelona, kwa sasa anakitumikia kikosi cha timu ya As Arta/Solar 7 ambacho kipo hapa Dar es Salaam kikijiandaa na msimu mpya hususan Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo kitakutana na Al Merrikh ya Sudan katika hatua ya awali ya michuano hiyo.

AS Arta/Solar 7 inatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Simba Septemba 3, mwaka huu, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Song alisema halifahamu vizuri soka la Tanzania ila alikuwapo katika Kilele cha Simba Day na kuona jinsi Watanzania wanavyopenda soka na timu yao.

Alisema kuhusu wachezaji wa Simba aliowaona siku hiyo wakati wakicheza mechi ya kirafiki dhidi ya St. George ya Ethiopia, alisema ni wazuri na anaamini wengi wao wana nafasi ya kucheza soka nje ya Afrika na kwamba kikubwa wanatakiwa kupambana na kujituma.

"Sijawahi kulifuatilia soka la Tanzania, sherehe za Simba nilifanikiwa kushuhudia mechi yao ya kirafiki dhidi ya St. George ya Ethiopia, kilichonivutia ni kuona mashabiki wengi kujitokeza na kujaza uwanja, hii ni ishara ya Watanzania kupenda cha kwao, lakini nimeona wachezaji wazuri na wakijituma zaidi watapata nafasi ya kucheza soka nje ya Afrika.

"Nina imani kufika kwetu kucheza soka Ulaya kunachangiwa na kuwasikiliza waliotuzidi, kuwa makini, kujituma, kufuata yale tunayopewa na kocha pamoja na kuhakikisha unathamini ile nembo ya jezi unayotumikia, ndiyo sababu kubwa ambayo imetufanya kufanikiwa na kucheza klabu mbalimbali Ulaya," alisema Song.

Kuhusu kurejea Afrika na kucheza ndani ya kikosi cha timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu ya Djibouti, alisema ni kwa sababu ya kutaka kuendelea kuacha uzoefu na kutoa somo kwa baadhi ya wachezaji vijana ili kufikia malengo yao.

"Huku ukanda wetu wa Afrika ni nchi chache sana ambazo wachezaji wanatoka katika kituo cha soka, wengi wao hawana misingi ya soka kuanzia chini sasa kuwapo kwangu hapa katika Klabu ya AS Arta Solar ni kutoa somo kwa vijana na kuwaeleza ni namna gani ya kufikia malengo yao ya kucheza soka kama ilivyo kwangu," alisema Song ambaye katika klabu hiyo yupo na nyota wa zamani wa Chelsea, raia wa Ivory Coast, Solomon Kalou.

## Stars njiapanda kufuzu CHAN

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa dakika nne kabla ya mechi kumalizika na straika wa Uganda 'The Cranes', Travis Mutyaba, jana liliiweka Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars kwenye njiapanda ya kufuzu kwa fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wanaocheza Ligi za Ndani (CHAN), zitakazofanyika mwakani nchini Algeria.

Yalikuwa ni makosa ya beki wa kulia, Mohamed Hussein 'Tshabalala', ambaye badala ya kuutoa mpira nje, alitaka kumgeuza kwa kumpiga changa mfungaji, lakini alizidiwa nguvu akaanguka, kabla ya mchezaji huyo kuondoka na mpira, akamdanganya Kibwana Shomari kama anapiga, lakini hakufanya hivyo akisababisha kunguka, kabla ya kutandika shuti kali la mguu wa kushoto lililotinga wavuni.

Pamoja na dakika nne zilizobaki, Stars kuonekana kama ndiyo wameamka kutoka kwenye usingizi mzito, lakini mabeki warefu wa Uganda wakiongozwa na Livingston Mulondo walikaa imara kuondosha hatari zote na hadi mwisho wa mchezo huo uliochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Stars ilikubali kipigo cha bao 1-0.

Majaliwa ya Stars kufuzu kwenye fainali hizo yatafahamika wiki ijayo Septemba 3, timu hizo zitakaporudiana nchini Uganda.

Kwenye mechi ya jana, Stars haikucheza vema, huku vijana wa Mserbia Milutin Sredojevic 'Micho', ambaye ni kocha wa zamani wa Yanga, wakionekana kutawala muda mwingi wa mchezo.

Straika hatari Milton Karisa alianza kulisalimia lango la Stars dakika ya nne tu ya mchezo, alipopokea mpira wa krosi kutoka winga ya kushoto akaachia kombora kali lililopaa juu ya lango.

Waganda walionekana kusaka bao la mapema, huku Stars ikiwa haijui nini inataka kufanya uwanjani na haikushangaza, Karisa, anayeichezea Vipers ya Uganda, alipopata tena pasi dakika ya 19 kutoka kwa Mulondo akachia shuti ambalo pia lilipaa juu la lango.

Stars haikuonekana kuwa na njia bora ya kuipita ngome ya Uganda Cranes, kwani mipira yao yote iliishia miguuni mwa mabeki wa timu hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >